‘CAG akague fedha akaunti ya amana halmashauri zote’
UKURASA 3



Vurugu zaibuka katika uchaguzi wa naibu meya
UKURASA 4



UKURASA 17
Israel yarusha mabomu mazito, hofu yatanda

Nipashe
MWANGA WA JAMII
Jumapili Oktoba 29, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • No. 0581478
www.ippmedia.com
JUMAPILI
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

UKURASA 22



JOSE MOURINHO KUONDOKA ROMA

# Posho za lishe kuponza vigogo

• **Rais** Samia aonya, mikoa hatari zaidi kwa udumavu, mimba za utotoni yaanikwa...

*Endelea Ukurasa 2*

**YALIYOMO**

UKURASA WA 11
**KWA NINI POMBE NI TISHIO HATIMA YA VIJANA WENGI?**




KARIBU tena msomaji tuangazie unywaji wa pombe. Ni eneo linalotesa sana watu wengi na hasa vijana...



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza jambo, baada ya kuzindua magari ya kubebea wagonjwa na magari ya usimamizi shirikishi, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu. **PICHA: IKULU**

## Ajali ya gari ilivyokatisha uhai msaidizi wa askofu

UKURASA 4



## Serikali yakunjua makucha yanayojiri huduma ‘massage’

UKURASA 2

MICHEZO GAMONDI AELEKEZA HESABU MSIMBAZI UK.24 MAONI, KATUNI UK.6




Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akimpongeza mbunifu wa kinu cha kufua chuma, Reuben Mtitu (kushoto), wakati alipotembelea banda lake katika maonyesho ya nne ya SIDO Kitaifa katika Uwanja wa Sabasaba mkoani Njombe jana. **PICHA: OMR**

# Posho za lishe kuponza vigogo

**Na Beatrice Shayo**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameonya wakuu wa mikoa kulipana posho za vikao kwa kutumia fedha za bajeti ya lishe huku udumavu ukiendelea katika maeneo yao, akiagiza mikoa yenye tatizo hilo wajitathmini.

Ni maelekezo aliyoyatoa jana jijini Dar es Salaam alipozindua Ripoti ya Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria Tanzania ya Mwaka 2022 na ugawaji wa magari ya kubeba wagonjwa na vifaa tiba.

Rais alisema ripoti inaonesha watoto 300 kati ya 1,000 kwenye jamii wana udumavu, akitaja ni kiwango kikubwa chenye tafsiri kwamba theluthi moja ya watoto wako katika hali ya udumavu.

"Wakuu wa mikoa tumetiliana mikataba ya lishe. Sasa haya matokeo yanayooneshwa hapa wakati tulitia saini mikataba tunakwenda kushughulika na taarifa imetuambia bajeti ya lishe imeongezeka kutoka ilivyokuwa.

"Kama mnatumia bajeti ya lishe kulipana vikao vya lishe ama posho, hebu badilisheni mtindo, bajeti iende kwenye afua kuliko kwenye kulipana posho za vikao. Niwaombe sana mkalishughulikie hili. Ni aibu kuwa na watoto wenye udumavu, tutakuja kuwa na taifa (ambalo) robo ya watu hawaelewi, sio hali nzuri," alionya.

Rais alisema kinachosikitisha zaidi, mikoa yenye viwango vya juu vya udumavu ni Iringa asilimia 57, Njombe (50), Rukwa (50) na Geita (39) ilhali mikoa hiyo inasifika kwa kilimo cha mazao karibu yote.

Rais Samia pia aliagiza suala la udumavu lichukuliwe kwa uzito mkubwa kwa ustawi wa jamii na usalama wa nchi, akitajaa athari za muda mrefu za udumavu ni kupunguza uwezo wa watoto kujifunza na kuongeza hatari kwa watoto kupata changamoto ya afya ukubwani na kuathiri nguvu kazi ya taifa.

Mkuu wa Nchi aliagiza: "Wakuu wote wa mikoa ambayo iko nyuma kuzuia mimba za utotoni na ile yenye viwango vikubwa vya udumavu wajitathmini na kuweka mikakati ya kubadilisha hali hiyo."

**VIFO VYA UZAZI**

Rais Samia alisema shabaha ya malengo ya maendeleo endelevu, ifikapo mwaka 2030 vifo vitokanavyo na uzazi visizidi 70 kwa kila vizazi hai 100,000, lakini hadi sasa nchini kuna wastani wa vifo 104 kwa kila vizazi hai 100,000.

"Safari yetu hadi ifikapo 2030 tunaweza kufikia, mwelekeo wetu ni nzuri. Wauguzi, madaktari na wakunga tusibweteke, twendeni tukaze mwendo, vifaa vipo, tukafanye kazi kuokoa uhai wa wenzetu," aliagiza.

Alisema ripoti hiyo imeonesha kupungua vifo vya watoto chini ya miaka mitano. Vilikuwa 67 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2015/16 na sasa kuna wastani wa vifo 45 kwa kila vizazi hai 1,000.

"Kwa upande wa vifo vya watoto wachanga hapa bado tuna kazi ya kufanya kwa sababu tumepunguza kwa asilimia moja. Hapa inawezekana kabisa hatukuwa na vifaa.

"Kuna kipindi Mungu alitaka nikaone kinachotokea kule kwa watoto njiti, nilipata kijukuu kikawa kimezaliwa kabla, nilipokwenda kumwangalia hospitalini, nilikuta hali ambayo ilinitoa machozi tena, kwa mara nyingine mashine hakuna, 'vitoto' vimepangwa kwenye mashine moja, vipo vingi vinalia na vingine vimewekwawekwa.

"Ninakata kukiona cha kwangu kimewekwa juu ya meza kanapigwa na taa juu, nikasema 'mbona mmemweka hapa?' Nikaambiwa ndio anapata joto, yaani anapata uhai wake. Nikasema hii hali hairidhishi," alisema.

Alisema hivi sasa wamegawa vifaa 123 vya watoto njiti na bado wameelezwa kuna hospitali 80 bado hazijapata na hospitali za mikoa nne.

Alisema kwa mujibu wa shabaha iliyowekwa na Umoja wa Mataifa, ifikapo mwaka 2030 idadi ya vifo vya watoto wachanga havitakiwi kuzidi 12 katika kila vizazi 1,000 na Tanzania bado navyo 24 kwa kila vizazi hai 1,000.

Rais Samia alisema ripoti hiyo imeonesha mafanikio katika kupunguza kiwango cha mimba za utotoni. Mikoa inayoongoza kuwa na kiwango kikubwa cha mimba za utotoni ni Songwe asilimia 45, Ruvuma (asilimia 37), Katavi (asilimia 34), Mara (asilimia 31) na Rukwa (asilimia 30).

Alibainisha kuwa mikoa ya Dar es Salaam, Njombe na Ruvuma viwango vya mimba za utotoni vimeongezeka. Dar es Salaam kutoka asilimia 11.9 hadi asilimia 18.1 na Njombe wametoka asilimia 19.7 hadi asilimia 25.5 .

"Mkajitazame Ruvuma wametoka asilimia 32 wamekwenda asilimia 37.2, mkaangalie nini chanzo cha hilo tatizo mfanyie kazi. Ninatoa wito kwa wazazi wenzangu tuendelee kuwalinda mabinti zetu wasiingie kwenye mitego ya mimba za utotoni," aliagiza.

Vilevile, Rais alisema ripoti imebainisha ongezeko la wajawazito wanaojifungulia kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kutoka asilimia 63 na kufikia asilimia 81.

Alielekeza Tume ya Mipango itumie matokeo ya ripoti hiyo katika maandalizi ya Dira mpya ya Maendeleo ya Taifa na mipango mbalimbali ya kitaifa.

Rais pia alikabidhi magari ya kubeba wagonjwa na ya usimamizi shirikishi, vifaa tiba kwa halmashauri mbalimbali, akiagiza wakasimamie vitumike inavyotakiwa na kuboresha huduma za afya.

Waziri Afya, Ummy Mwalimu, alisema Rais Samia ameonesha utashi katika suala la uzazi kwa mama na mtoto kwa kuwa kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi, akikumbusha kuwa vilikuwa 30 kwa siku mwaka 2017 na kwa sasa vimepungua kutokana na jitihada kubwa alizozifanya.

Alisema hivi karibuni wataanza kupokea wagonjwa wa saratani kutoka Zambia. Watatibiwa katika Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI).

## Serikali yakunjua makucha 'massage'

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, ametangaza kusitishwa huduma za kituo cha kuchua (massage) cha Tia Smile and Spa kilichoko Mtaa wa Nzasa, Kijitonyama, Dar es Salaam kutokana na kutokidhi viwango kisheria.

Hatua hiyo imechukuliwa na serikali baada ya kusambaa video fupi mtandaoni iliyotolewa na Gerald Komba, akilalamikia tangazo la biashara ya huduma ya 'massage', akiwa na madai kwamba huduma zinazotolewa huko ziko kinyume cha maadili.

Komba alihoji iwapo serikali imeridhia tangazo hilo huku akimtaja Waziri Dorothy na kumwomba achukue hatua.

Waziri Dorothy alisema kuwa baada ya video hiyo kusambazwa, hatua alizochukua kwa kushirikiana na wananchi, alibaini ilirekodiwa Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam.

"Niliwasilisha taarifa hiyo kwenye mamlaka ya mkoa na kuelekeza hatua stahiki zichukuliwe. Hatua zilizochukuliwa na mamlaka ya mkoa ni huduma husika imesitishwa kuanzia Oktoba 26 mwaka huu.

"Imesitishwa kutokana na kutokidhi viwango vya Sheria Na. 23 ya Mwaka 2002 ya Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala na mmiliki ametozwa faini ya Sh. 500,000 kwa mujibu wa sheria. Amepewa maelekezo ya kufuata, vinginevyo atapelekwa mahakamani," alisema Waziri.

Alisema wako baadhi ya watoa huduma wasiotimiza matakwa ya sheria za huduma wanazotoa, hivyo kuathiri maendeleo na ustawi wa jamii, ikiwamo kuchochea mmomonyoko wa maadili.

Waziri Dorothy alisema hali hiyo huchangia kuibuka matukio ya unyanyasaji na udhalilishaji wa kijinsia, watoto wakiwa waathirika zaidi.

Waziri huyo pia alisema watafanya mazungumzo na wadau, wamiliki na watoa huduma za kisekta kuhusu changamoto zinazowazuia kutimiza matakwa ya kisheria wakati wa kutoa huduma na kutoa taarifa.

"Ninatoa shukrani kwa aliyetoa taarifa hizi kwani ameonesha uzalendo kwenye kuona tatizo au changamoto na kuchukua hatua.

"Shukrani kwa Mamlaka ya Mkoa na Serikali za Mitaa pamoja na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni kwa ushirikiano na wepesi wa kuitikia na kuchukua hatua stahiki. Shukrani kwa wananchi wote ambapo wameendelea kutoa ushirikiano," alisema.

Waziri huyo alitoa wito kwa Watanzania wengine wote kuchukua hatua stahiki pale wanapoona kuna jambo ambalo halina tija kwa maendeleo na ustawi wa jamii.

"Iwapo kuna haja ya rufani wizarani; jamii itumie kituo cha huduma kwa wateja simu: 0734 986503 na 026 2160250.

"Kuhusu ukatili kwa watoto, wapige simu na 116 saa 24 kila siku bila malipo. Iwapo waziri mwenye dhamana atahitajika, tuma ujumbe kwenye kwa namba 0765 345777 au 0734 124191," alisema.



Ofisa Mnadhimu wa Polisi Kikosi cha Wanamaji Tanzania, SSP Shomari Jumbe, akizungumza na wavuvi wanaofanya shughuli zao katika ufukwe wa Kunduchi, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, kuhusu kuacha matumizi ya nyavu za kokoro na baruti kwani zinahatarisha usalama wao na mazalia ya samaki na kuwataka wafanye uvuvi salama pamoja na kuzuia uhalifu ili kijiongezea fursa ya kipato halali kutokana na mazao ya bahari. **PICHA: MAULID MMBAGA**

RIPOTI YA UHAMISHAJI FEDHA

# 'CAG akague fedha katika akaunti ya amana halmashauri zote nchini'

**Na Mwandishi Wetu**

SIKU chache baada ya kutolewa ripoti ya uchunguzi wa tuhuma za ubadhirifu wa fedha kwenye Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji, Chama cha ACT Wazalendo kimesema kuna haja kufanyika ukaguzi maalum katika akaunti za amana za halmashauri zote nchini.

Chama hicho kimependekeza hilo, kikieleza kuguswa na kuumizwa na taarifa ya kukithiri vitendo na mtandao wa ubadhirifu wa fedha za umma katika halmashauri mbalimbali nchini.

Mnamo tarehe 25 Oktoba mwaka huu, Ofisi ya Waziri Mkuu ilitoa taarifa kwa umma kuwa matokeo ya uchunguzi wa tuhuma za ubadhirifu wa fedha kwenye Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji yamebainisha kuwapo mtandao wa uhamishaji fedha kinyume cha taratibu.

Taarifa hiyo ilieleza kubainika kuwapo ubadhirifu mkubwa wa fedha za umma kupitia kitengo cha usimamizi wa fedha katika Akaunti Jumuifu ya Amana kilichoko TAMISEMI kwa kushirikiana na halmashauri mbalimbali nchini.

Sehemu ya taarifa hiyo inasema: "Timu imebaini kuwa Kitengo cha Usimamizi wa Fedha katika Akaunti Jumuifu ya Amana kilichopo TAMISEMI kinahusika kutuma fedha kwenye halmashauri mbalimbali na kisha kuzitoa kwa kushirikiana na watumishi wa halmashauri hizo."

Kulthumu Mchuchuli, Waziri Kivuli wa ACT -Wazalendo - TAMISEMI na Maendeleo Vijijini, katika taarifa yake kwa vyombo vya habari jana, alisema kuwa licha ya kutolewa taarifa hiyo, hakuna hatua zilizoelezwa kuchukuliwa ili kukabiliana na mtandao huo wa ubadhirifu unaendelea kwenye halmashauri nchini.

"ACT Wazalendo inaamini kuwa matokeo ya uchunguzi ya Manispaa ya Kigoma Ujiji ni sampuli tu ya kile kinachoendelea kwenye halmashauri mbalimbali nchini.

"ACT Wazalendo tunatoa wito kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kufanya ukaguzi maalum wa fedha katika akaunti ya amana katika halmashauri zote nchini.

"Pia serikali iwasimamishe kazi watendaji wanaohusika na usimamizi katika kitengo cha akaunti ya amana kilichoko Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI)," alisema.

**CAG, WATAALAMU**

Ripoti ya Uwajibikaji ya Viashiria vya Rushwa, Ubadhirifu na Udanganyifu 2021/22 iliyoandaliwa na Taasisi ya WAJIBU kutokana na ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) za ukaguzi wa Serikali Kuu, Mashirika ya Umma na Mamlaka ya Serikali za Mitaa za mwaka wa fedha 2021/22, inabainisha miamala mbalimbali yenye viashiria vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu wa fedha za umma.

Kwa mwaka wa fedha 2021/22, uchambuzi umeonesha kuna viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu katika matumizi ya kawaida, mishahara, mafao na rasilimali watu yenye thamani ya Sh. bilioni 411.31 yaliyotokana na kasoro mbalimbali.

Dosari hiyo imepungua kwa asilimia 63 kutoka Sh. trilioni 1.14 mwaka wa fedha 2020/21 mpaka Sh. bilioni 411.31 mwaka wa fedha 2021/22.

Mathalani, katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa (halmashauri),

Kasoro zaidi zilizobainishwa kuwa na viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu ni pamoja na halmashauri 19 zilifanya ununuzi wenye thamani ya Sh. bilioni 14.02 nje ya mpango wa ununuzi wa halmashauri husika.

Ni tatizo linaonekana kuongezeka ingawa idadi ya halmashauri imepungua. Kwa mwaka 2020/21, halmashauri 24 zilifanya ununuzi wenye thamani ya Sh. bilioni 3.84 bila kuzingatia mpango wa ununuzi wa halmashauri husika.

Pia upo ununuzi wenye thamani ya Sh. bilioni 7.45 ulifanyika katika halmashauri 45 za serikali za mitaa bila kuitisha nukuu za ushindanishi wa bei.

Baadhi ya Mamlaka ya Halmashauri zilizokuwa na kiasi kikubwa ni pamoja na: Wilaya ya Kaliua Sh. milioni 894.82, Wilaya ya Missenyi Sh. milioni 648.60, Wilaya ya Bunda Sh. milioni 576.04 na Wilaya ya Momba Sh. milioni 445.07.

Kuna tatizo lingine la mikataba iliyotiwa saini bila kuhakikiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali yenye thamani ya Sh. bilioni 6.68 kwenye halmashauri 20.

Upungufu pia ulionekana katika dhamana za utendaji wa mikataba ya miradi ya ujenzi yenye thamani ya Sh. bilioni 7.64 katika halmashauri 10. Mfano wa upungufu huo ni kuwapo dhamana ya utendaji uliyoisha muda wake katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha.

## Mpango akaribisha uwekezaji kushusha gharama za umeme

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango amewataka wadau kujitokeza kuwekeza kwenye miradi ya nishati ya umeme ili kuhakikisha nchi inakuwa na umeme wa kutosha, uhakika na wa bei nafuu.

Akizindua mradi wa umeme wa ELCT Ijangala Hydropower Plant wa kilowati 360 katika Kijiji cha Masisiwe wilayani Makete, mkoani Njombe juzi, Dk. Mpango alisema upatikanaji umeme wa uhakika ni kichocheo cha maendeleo ya watu na taifa.

Mradi huo ambao unamilikiwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Kusini Kati, una thamani ya zaidi ya Sh. bilioni tatu.

"Sasa ili tufike hapo, tunahitaji uwekezaji imara na katika uzalishaji, usafirishaji na nishati ya umeme katika maeneo ya uzalishaji na usindikaji bidhaa," alisema Dk. Mpango.

Kiongozi huyo aliagiza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kulipa fidia wananchi wanaopisha mradi wa umeme wa Rumakali unaotarajiwa kuzalisha megawati 204 katika Kijiji cha Madihani wilayani humo.

Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga, alisema wataendelea kufanya kazi kwa bidii ili kuhakikisha vijiji vyote vinafikiwa na nishati hiyo.

"Wilaya ya Makete wanakaribia kumaliza kupeleka umeme kwa vijiji vyote 98, tunategemea hadi kufika Oktoba 30 mwaka huu, tutakuwa tumepiga hatua ili megawati 80 zote za mradi wa Rusumo ziweze kuingia kwenye Gridi ya Taifa.

"Kupitia REA (Wakala wa Nishati Vijijini) na TANESCO, tunatekeleza miradi nishati mbalimbali ikiwamo miradi ya kuzalisha pamoja na kusafirisha umeme, si tu ndani ya nchi yetu, lakini kwa kuunganisha nchi nyingine jirani kama Zambia, Kenya, Uganda, Burundi na Malawi," alisema.

Mkuu wa Dayosisi ya Kusini Kati, Askofu Wilson Sanga alisema mradi huo ulianza kwa utafiti mwaka 2010 na ujenzi wake ulianza rasmi Machi 2021 kama shughuli ya kwanza ya Nishati Lutheran (DKK) Investment Limited, kampuni iliyoanzishwa na dayosisi na kusajiliwa kwa mujibu wa sheria za nchi. "Kwa sasa mradi unazalisha umeme wa kilowati 360 na umeunganishwa na Gridi ya Taifa (National Grid) kwa kufuata makubaliano ya kimkataba kati ya TANESCO na Nishati Lutheran (DKK) Investment Limited yaliyotiwa saini Desemba 2020.

"Hiyo ni kutokana na fursa zilizopo kwenye chanzo ingawa kinaweza kutoa umeme wa hadi megawati mbili iwapo mitambo itaongezwa," alisema.

Askofu Sanga alisema REA imetoa ruzuku na imeendelea kuchangia sehemu ya gharama za ujenzi ambapo Sh. milioni 997.5 zimetolewa pamoja na mkopo nafuu kupitia Benki ya Maendeleo (TIB) - Dola za Marekani 400,000 sawa na zaidi ya Sh. milioni 850.

Meneja wa Teknolojia za Nishati Vijijini kutoka REA, Michael Kessy, alisema wametoa Sh. milioni 997 kwa awamu tatu tofauti ili kufanikisha mradi huo.

"Awamu ya kwanza ilikuwa katika maandalizi ya mradi ambapo wakala ulisaidia kuandika andiko la mradi pamoja na mpango biashara na pia kuandika andiko la athari za jamii za kimazingira, REA pia ilishiriki katika ujenzi," alisema Kessy.

Awali, Mbunge wa Makete, Festo Sanga, alimweleza Dk. Mpango changamoto ya ucheleweshwaji madai ya fidia kwa wananchi wanaopisha mradi wa umeme wa Rumakali ulioko katika Kijiji cha Madihani.

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geofrey Pinda, alisema utolewaji hati za hakimiliki za kimila unafuatia uwezeshaji wa uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji uliofanywa na wizara yake kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (NLUPC).

# Vurugu zaibuka uchaguzi Naibu Meya

**Na Vitus Audax,** MWANZA

UCHAGUZI wa Naibu Meya wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza, umegubikwa na vurugu na kelele jambo lililosababisha walinzi kuwatoa nje baadhi ya wajumbe waliokuwa wakipiga kelele kupinga uchaguzi huo unaodaiwa una hujuma.

Vurugu hizo zilitokea juzi baada ya Meya wa Jiji, Sima Constantine Sima, na Mkurugenzi wa Jiji, Aron Kagurumjuli, kusoma jina tofauti na lililopitishwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) ili kupitishwa na Baraza la Madiwani.

Diwani wa Milongo, Hamidu Said, ambaye alishinda katika kura za maoni, akizungumza katika baraza hilo, alisema akiwa mteule wa nafasi hiyo anashangazwa kutajwa jina la mwezake aliyeshika nafasi ya pili kwenye kura hizo.

"Nashangazwa kwa nini baraza limeletewa jina tofauti ilihali mimi ndiye niliyeshinda na sijapokea barua yoyote ya utenguzi wangu wala hakuna sababu zozote zilizotolewa kuhusu suala hilo," alisema. Pia alieleza kutokukubaliana na uchaguzi huo kwa kile alichodai kuwa umekiuka kanuni na taratibu zilizowekwa kwa kuwa angekuwa ametenguliwa, ilitakiwa apate barua ya aliyeshinda kuwania nafasi hiyo.

Akitoa ufafanuzi kuhusu sintofahamu hiyo, Kagurumjuli alisema wakiwa serikali wanapokea taarifa kutoka kwenye chama husika na kuiwasilisha katika baraza kwa ajili ya hatua ya mwisho.

Alisema masuala yote yanayohusiana na michakato ya chama hawahusiki nayo kwa kuwa wanatoa nafasi kwa chama kupendekeza jina na kuwasilishwa kwenye halmashauri, hivyo hawewezi kueleza sababu za chama hicho kuleta jina tofauti na la aliyeshinda katika kura za maoni.

"Tungekuwa na vyama vitatu au zaidi basi vingewasilisha barua za kutambulisha wagombea wao kama ilivyo kwa chama hiki, hivyo hatuwezi kuingilia uamuzi wa chama chochote," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema kama kuna mchakato au kanuni zilizokiukwa na chama husika ni wajibu wa mtendewa kupeleka malalamiko yake kwenye chama na si halmashauri.

Hata hivyo, Diwani Hamidu hakuridhishwa na majibu hayo na kumtaka Mstahiki Meya kutoa ufafanuzi juu ya sababu zilizofanya jina lake kuondolewa na kuletwa jina la Bhiku Kotecha aliyekuwa mshindi wa pili katika kura za maoni. Sima alifafanua kuwa haijalishi kuna ukanyagwaji wa haki katika chama husika lakini chama kimepewa mamlaka ya kuwasilisha jina halmashauri na hawawezi kujadili masuala ya chama.

Hata hivyo, uchaguzi uliendelea licha ya baadhi ya wajumbe wa mkutano kususia huku wengine wakipigana nje ya ukumbi. Kura zilipigwa za Ndiyo au Hapana na Kotecha kupata kura 20 zilizomkubali huku mbili zikimkataa.

# Ajali ya gari ilivyokatisha uhai wa msaidizi wa askofu

**Na Elizabeth John,** NJOMBE



MSAIDIZI wa Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Kusini, Mchungaji Dk. Gabriel Nduye (58), (pichani) amefariki dunia kwa ajali ya gari.

Dk. Nduye alikutwa na mauti kwenye ajali iliyotokea katika kijiji cha Ng'anda, barabara ya Njombe-Makete, alipokuwa akienda kwenye Kongamano la Sita la Wainjilisti wa Jimbo la Njombe la Dayosisi hiyo.

Katibu Mkuu wa Dayosisi ya Kusini, Grayson Shilongoji, alisema jana kuwa walipokea taarifa ya kifo cha kiongozi huyo Alhamisi majira ya saa 10:00 jioni.

"Taarifa hii tuliipokea kwa mshtuko mkubwa kwamba amepata ajali katika kijiji cha Ng'anda. Alikuwa ametoka huku Njombe mjini akienda kuungana na watumishi wengine ambao walikuwa wameenda naye asubuhi huko Ng'anda ambako kulikuwa kukifanyika kongamano la wainjilisti.

"Kwa hiyo alifika huko asubuhi na akawa na kipindi chake cha asubuhi. Baada ya hapo, akarudi huku Njombe kukabili jambo la kifamilia kumhudumia baba yake mzazi kumpeleka pale Hospitali ya Rufani ya Mkoa kwa ajili ya kliniki, akatekeleza jukumu hilo na kumrudisha nyumbani.

"Baada ya hapo aliona aende kuungana tena na watumishi wenzake kule Ng'anda akiwa na kipindi cha hiyo jioni. Alipokuwa akienda huko, mwendo kidogo kabla ya kufika ikawa imetokea hiyo ajali ya lori la mbao na gari letu la kanisa ambalo alikuwa akiendesha," alisema Shilongoji.

Akimwelezea Mchungaji Dk. Nduye, alisema: 'Nilimfahamu kama mtu ambaye ni mchapakazi, mtu wa kujituma sana, mvumilivu, asiyekata tamaa na hapa ninasema hivyo kwa sababu aliweza kuwafundisha vijana kule Chunya katika mambo ya uimbaji kwa kitaalamu"alisema.

**KAULI YA ASKOFU**

Askofu wa KKKT Dayosisi ya Kusini, Dk. George Fihavango, alisema alipokea kwa mshtuko taarifa ya kifo cha msaidizi wake.

"Sijaamimi ninachoambiwa kwa sababu asubuhi siku ya tukio tulikuwa na kikao kifupi. Tulikuwa tunagawana majukumu, mwenzangu anakwenda kwenye semina Ng'anda na mimi naendelea na majukumu mengine halafu baadae napigiwa na mtunza hazina anasema Msaidizi wa Askofu amepata ajali. Nauliza anaendeleaje akasema wazi amefariki dunia "alisema.

Kuhusu mazishi, Askofu Dk. Fihavango alisema Mchungaji Dk, Nduye anatarajiwa kuzikwa kesho kijijini kwao Ukalawa, Lupembe mkoani Njombe.

Alisema mwili wa marehemu utatolewa leo katika Hospitali ya Ilembula inayomilikiwa na kanisa hilo na kupelekwa nyumbani kwake eneo la Kambarage, mjini Njombe kuanzia saa 9:00 alasiri. Saa 11:00 jioni, alisema mwili utapelekwa Kanisa Kuu la Dayosisi mjini Njombe kwa maombolezo na mkesha usiku kucha.

Kesho asubuhi, alisema kutafanyika ibada kanisani hapo kabla ya kuanza msafara kwenda kijijini kwao Ukalawa, Lupembe kwa maziko.

Katibu Mkuu Msaidizi wa Dayosisi ya Kusini, Petro Kilima, alisema Mchungaji Dk. Nduye atamkumbuka kwa mambo mengi aliyoyafaya wakati wa uhai wake.

"Amefanya kazi nyingi sana na muda mwingi amefanya kazi ya kujitoa. Amekuwa na moyo wa uvumilivu sana katika mazingira mengi na alipenda sana kuwasaidia watu," alisema.

**HISTORIA YAKE**

Mchungaji Dk. Gabriel Nduye alizaliwa Desemba 25, 1965 Ukalawa, Lupembe mkoani Njombe. Alibatizwa Januari, 1966 na kupata kipaimara Desemba, 1982 na Mchungaji Goden Kitaponda.

Alipata elimu ya msingi mwaka 1976 hadi 1982 katika Shule ya Msingi Ukalawa na elimu ya sekondari mwaka 1995-1998 akiwa mtahiniwa wa kujitegemea Chuo cha Ualimu Kleruu, Iringa na kidato cha sita kama Mtahiniwa wa kujitegemea.

Mwaka 1989 hadi 1992 alijiunga na kozi ya uinjilisti ngazi ya cheti katika Chuo cha Theologia Kidugala na mwaka 1996 hadi 2000 kozi ya Diploma ya Theologia Chuo Kikuu Kishiriki cha Tumaini Iringa (sasa Chuo Kikuu cha Iringa) mwaka 2002 hadi 2004.

Alijiunga na masomo ya Shahada ya Kwanza ya Theolojia katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Tumaini Iringa mwaka 2005-2006 na Stashahada ya Uzamili katika uongozi katika chuo hicho.

Kiu yake ya kujiendeleza kitaaluma haikuishia hapo kwani alijiunga na Chuo Kikuu cha Kwazulu Natal, Afrika Kusini na kuhitimu shahada ya kwanza ya Theolojia na Maendeleo mwaka 2011. Aliendelea na masomo katika chuo hicho kwa shahada ya uzamili katika theolojia na maendeleo na kuhitimu mwaka 2012.

Aliendelea na masomo katika chuo hicho kwa masomo ya shahada ya uzamivu (PhD) katika theolojia na maendeleo na kuhitimu mwaka 2015.

Dk. Nduye aliajiriwa na Dayosisi ya Kusini mwaka 1992-1993 akiwa Mwinjilisti mtaa wa Chunya Mjini mwaka Usharika wa Chunya. Mwaka 1993-1996 alikuwa ,Katibu wa Idara ya Vijana Jimbo la Lupembe na Septemba 10, 2000 alibarikiwa kuwa Mchungaji na Askofu Zephania Mgeyekwa (sasa marehemu). Mwaka 2000-2002 alikuwa Mchungaji Kiongozi Usharika wa Tumaini, Jimbo la Mufindi (sasa Dayosisi Teule ya Mufindi).

Mwaka 2006 hadi 2009 alikuwa Mratibu Mkazi wa Udugu kati ya Dayosisi ya Kusini na Sinodi ya Western Iowa ya Marekani na mwaka 2015 baada ya kuhitimu shahada ya uzamivu, aliendelea na wajibu huo na Meneja wa Mradi wa Maendeleo ya Kilimo Lupembe(Centre for Agricultural Development-CAD)

Mwaka 2017-2019 alikuwa Mkuu wa Jimbo Makambako na Mei 8, 2019 alichaguliwa kuwa Msaidizi wa Askofu, nafasi aliyoitumikia hadi anafariki dunia.

Mchungaji Nduye alioana na Grace Mponzi na kujaliwa kupata watoto wanne, wa kike watatu na wa kiume mmoja.


IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA
MISC. LAND CASE APPLICATION No. 38 OF 2023
KOMBO MUSSA ITASO......APPLICANT
VERSUS
METHEW KIZA ELGAS.......RESPONDENT

TO METHEW KIZA ELGAS
NOTICE OF DATE OF MENTION:

**TAKE A NOTE** that the above case has been fixed for hearing/ Mention on the 31 Day of October 2023 at 9:00 am. Before **Hon. MPELEMBWA .......**RM/SRM.
**YOU ARE** required to appear in this court on the fixed date without fail and you may bring with you all required documents in support of your case .
Given under my hand and the seal of the court this 25 Day of October 2023.
SENIOR RESIDENT MAGISTRATE



KUPOTEA KWA CHETI



SARAH DANIEL MWAIGOMEKO anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S3914/0101 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia ALFA GEMS SEKONDARI mwaka 2020. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: PHQ/DAR/KIG/29467/2023.



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika Mahakama ya Mwanzo ya BUGANDO
Wilaya ya GEITA
Mkoa ..................GEITA
Shauri la TALAKA Na 29/2023
Jina la Mdai: BAHANUZI DEOGRATIAS CHOMANGA
Jina la Mdaiwa: VERONICA DANIEL

KUITWA SHAURINI MDAIWA
(Kanuniya 18 ya kanun iza taratibu Madai katika mahakama za Mwanzo)

**Kwa: VERONICA DANIEL WA IGATE GEITA**
**AMRI:-** Unaamriwa na Jamuhuri uhudhurie Mahakamani hapa siku ya Jumanne tarehe 31/10/2023 saa 2:00 Asubuhi ili ujibu madai ya Talaka. Usipohudhuria kesi itasikilizwa bila wewe kuwepo
Unaonywa usikose kuhudhuria.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo Tarehe 23 Mwezi 10 Mwaka 2023
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
BUGANDO

## HABARI KITAIFA

UMEME WA RATIBA

# Wenye viwanda wafunguka kupata hasara ya mamilioni

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

WAMILIKI wa viwanda na migodi mkoani Singida wamelalamikia tatizo la kukosekana umeme wa uhakika kila siku ambalo limeathiri kwa kiwango kikubwa uzalishaji na kuwaingizia hasara ya mamilioni ya shilingi.

Malalamiko hayo yaliwasilishwa jana na wamiliki hao kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Dk. Binilith Mahenge, ambaye yumo mkoani humu kwa ziara ya siku mbili inayolenga kuhamasisha uwekezaji wa ndani.

Katika ziara hiyo, Dk. Mahenge alitembelea kiwanda cha kuchambua pamba cha Biosustain (T) Limited, viwanda vya kusindika mafuta cha Wild Flower, Grains and Oil Mill Project na Mount Meru katika Manispaa ya Singida na Mgodi wa Shanta Gold ulioko Wilaya ya Ikungi.

Mkurugenzi wa kiwanda cha kuchambua pamba cha Biosustain (T) Limited, Sajjiad Haider, alimweleza Mwenyekiti wa TIC kuwa 'umeme wa ratiba' umekuwa changamoto kubwa kwako.

Alisema walipokea barua kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwamba umeme utakatwa mara mbili kwa wiki, lakini sasa unakatwa hadi mara tatu kwa wiki.

"Tatizo hili ambalo limeanza mwezi Septemba mwaka huu, limeathiri uzalishaji kwa kiwango kikubwa na kusababisha hasara. Kwa siku unapokatwa tunakaa zaidi ya saa nane bila kuendelea na uzalishaji," alisema.

Haider alisema kutokana na tatizo hilo, uzalishaji pamba ambao matarajio yao yalikuwa ni hadi kufikia mwezi Novemba 2023, uwe umekamilika, kwa sasa itafika hadi Januari au Februari mwakani.

Alisema katika msimu huu wa kilimo, kiwanda hicho kimenunua zaidi ya tani 36,000 kutoka kwa wakulima wa mikoa ya Shinyanga, Simiyu na Singida. Mkoa wa Singida ulianza kilimo cha pamba mwaka 2017 na wakulima wake wamefikia uzalishaji wa tani 4,000 kutokana na uhamasishaji uliofanywa na kiwanda kwa kushirikiana na serikali.

Kaimu Meneja wa Mgodi wa Shanta Gold, Reuben Ngusaru, alisema umeme umekuwa changamoto kubwa kwenye mgodi huo na kuathiri uzalishaji ambapo wanapotumia jenereta gharama huwa kubwa.

Akitolea ufafanuzi kuhusu changamoto hiyo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TIC, Dk. Mahenge alisema kwa kuwa TIC ndio kimbilio la wawekezaji na ndiyo sauti yao, hivyo itahakikisha inawasiliana na wanaohusika na sekta ya nishati.

Alisema serikali inajitahidi kumaliza tatizo la umeme nchini. Mradi wa Kufua Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) utakapoanza, uzalishaji utaongeza kiwango cha uzalishaji umeme. Mradi huo unatarajiwa kuzalisha megawati 2,115.




Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Kokilaben Dhilirubhai Ambani ya India, Dk. Santosh Shetty (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu uzinduzi wa Kituo cha Hospitali ya Mumbai Health Service Ltd, kilichopo Oysterbay. Wengine ni Daktari Bingwa wa Saratani kutoka Kokilaben Dhilirubhai Ambani, Rajesh Mistry (Kulia), Mkurugenzi wa Kituo hicho, David Dickson (wa pili kulia) na Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Kituo hicho, Lillian Mwasha. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mwongozo elimu ya dawa za kulevya shuleni waandaliwa

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Tanzania (DCEA) imeandaa mwongozo wa vitabu shule na vyuo kwa ajili ya kufikisha elimu ya madhara ya matumizi ya dawa za kulevya kwa wanafunzi.

Hatua hiyo inatokana na utafiti kuonesha kuwapo kundi kubwa la wanafunzi wengi kujihusisha na dawa za kulevya.

Kamishna Jenerali wa DCEA, Aretas Lyimo, alibainisha hayo juzi wakati wa wasilisho la Taarifa ya Utendaji wa Mamlaka kwa Mwaka 2023/24 mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge, Utawala Katiba na Sheria bungeni jijini hapa.

Lyimo alisema wameamua kufanya hivyo ili kutoa elimu kwa wanafunzi ikiwamo kuwakumbusha madhara ya matumizi ya dawa za kulevya ili kuepuka kupoteza watoto ambao ni taifa la kesho.

"Tumeandaa mwongozo wa vitabu ambao unazungumzia madhara ya matumizi ya dawa za kulevya pamoja na rushwa," alisema.

Baadhi ya wajumbe wa Kamati hiyo walipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) kupitia DCEA kwa kazi nzuri ya mapambano dhidi ya biashara hiyo haramu.

Mjumbe wa kamati hiyo, Dk. Alice Kaijage, alisema mamlaka hiyo imekuwa inatekeleza mapambano dhidi ya dawa za kulevya kutokana na kuwapo mwongozo na mfumo wa mawasiliano wa kubadilishana taarifa na kuwa na utendaji mzuri.

"Mifumo ni muhimu sana kwa kubadilishana taarifa na taasisi nyingine na mchakato mzima wa kutoa taarifa kupitia mawasiliano ya simu," alisema Dk. Kaijage.

Alisema uanzishwaji wa vilabu vya wanafunzi katika shule za msingi na sekondari vinavyotumika kutoa ujumbe na mafunzo dhidi ya mapambano ya rushwa na dawa za kulevya, umesaidia kujenga uelewa kwa wanafunzi kutambua mchango wao katika mapambano hayo.

Pia alisema umewasaidia kufahamu madhara ya rushwa, matumizi ya dawa za kulevya na hatua za kuchukua ili kusaidia kutimiza ndoto zao. Aliipongeza mamlaka hiyo kwa kutumia vizuri fungu la fedha za maendeleo kwa kuanzisha nyumba za utengamao zinazosaidia warahibu kujifunza stadi mbalimbali zinazowasaidia kujiimarisha kiuchumi.

Akiwasilisha Taarifa ya Utendaji wa Mamlaka mwaka 2023/24 kwa kamati hiyo, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Ummy Nderiananga, alisema imetoa elimu kwa umma kuhusu madhara ya dawa za kulevya, mafunzo ya udhibiti wake, kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya kwa wadau na wataalamu wa dawa tiba, maduka ya dawa, asasi za kiraia na vituo vya forodha.

Nderiananga alisema mamlaka imetoa elimu kuhusu madhara ya kilimo cha bangi na mirungi katika maeneo yaliyokithiri mazao hayo katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Mara.

Pia alisema mamlaka ilitoa elimu kuhusu madhara ya biashara na matumizi ya dawa za kulevya kwa wakuu wa mikoa na makatibu tawala wa mikoa yote nchini.

## JKCI kujenga jengo jipya la huduma za moyo Mlongazila

**Na Christina Mwakangale**

TAASISI ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) inatarajia kujenga jengo jipya la moyo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH)-Mloganzila litakalotoa huduma kubwa zaidi ya Upanga.

Jengo hilo linatarajiwa kujengwa na taasisi hiyo kwa kushirikiana na Serikali ya China. Litagharimu Sh. bilioni 30.

Kaimu Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Dk. Tatizo Waane, alibainisha hayo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu ujenzi huo ambao utaanza mwakani.

Alisema Serikali ya China ilituma ujumbe ili kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi huo, ikiwamo eneo na matarajio ni kukamilika ndani ya miaka mitatu.

"Ujenzi unaweza kuanza mwishoni mwa mwaka huu au mwanzoni mwa mwaka ujao eneo la Mloganzila, na jengo linatarajiwa kutatoa huduma kubwa kuliko hapa Upanga JKCI, kwa kuwa eneo la pale ni kubwa na vifaa vya kutolea huduma vitaongezeka," alisema Dk. Waane.

Mwakilishi wa Wizara ya Afya, Dk. Liggyle Vumilia, alisema Tanzania na China zimekuwa zinashirikiana katika sekta mbalimbali na hatua hiyo ni mwendelezo wa ushirikiano huo.

Bingwa wa Magonjwa ya Moyo kwa Watoto na Mkuu wa Kitengo cha Uhakiki na Ubora kutoka taasisi hiyo, Dk. Naihizihijwa Majani, alisema kwa mwaka taasisi hiyo inahudumia takribani wagonjwa wa nje 500 kwa siku.

"Kwa mwaka tunafanya upasuaji unaofikia watu 400 na kuhudumia wagonjwa wa nje 500 na matarajio kwa taasisi itakayojengwa huduma zitaongezeka zaidi," alisema bingwa huyo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Utafiti kuhusu unywaji pombe uiamshe serikali

**"UKICHEKA** na nyani utavuna mabua." Msemo huu ni wa tahadhari kwa wakulima kuwa makini dhidi ya nyani kwenye mashamba yao kwa kuwa wasipochukua hatua, wanyama hao watakula mazao yote na kujikuta wanaambulia patupu.

Msemo huo kwa sasa unaihusu Tanzania kuhusu kizazi kijacho kuwa katika hali mbaya baada ya kutolewa taarifa ya utafiti kuhusu vijana na watoto kujihusisha na unywaji wa pombe wakiwa katika umri mdogo, wakiwamo wa chini ya miaka 15.

Taarifa hiyo ya utafiti inaashiria kwamba taifa linatishiwa na hatari ya ongezeko la kizazi kisicho na dira na matokeo yake kuwa na watu wasio na uwezo katika kufanya kazi kwa sababu ya matumizi ya pombe.

Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Wizara ya Afya mwaka 2018, kwa wanafunzi wa shule za sekondari mkoa wa Dar es Salaam, asilimia tano waligundulika kutumia pombe.

Utafiti huo pia unaonyesha kuwa vijana wanaoanza kutumia pombe wakiwa chini ya umri wa miaka 15, wako katika hatua ya kuwa na utegemezi mara sita zaidi ya wale wanaoanza kutumia vilevi hivyo wakiwa na miaka 21.

Aidha, utafiti huo ulionyesha kuwa asilimia 10.8 ya vijana walianza kutumia pombe kabla ya kufikisha umri wa miaka 14 huku asilimia 26.2 walikuwa na mzazi anayetumia pombe.

Kutokana na matokeo hayo, imebainishwa kuwa matumizi ya pombe wakati wa utoto na ujana, yanaweza kuwa na athari mbaya kiafya, kijamii, kiuchumi na kimaendeleo kwa vijana na jamii kwa ujumla.

Hatua hiyo imeiamsha kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) kuanza kampeni ya kutoa elimu shuleni kuhusu athari mbaya zinazotokana na utumiaji wa pombe katika umri mdogo.

Matokeo hayo ya utafiti hayana budi kuiamsha serikali na wadau kwa ujumla katika kutoa elimu kwa vijana na watoto kuhusu athari za matumizi ya pombe katika umri mdogo.

Kinyume cha hapo, kama utafiti unavyoonyesha, ni dhahiri kwamba kama hali itaachwa ilivyo, kuna hatari katika miaka ijayo kuwa na taifa la vijana mizigo ambao watakuwa wategemezi na wasio na uwezo hata wa kujitunza na hata kuwajibika katika familia.

Serikali inapaswa kuchukua hatua katika kudhibiti hilo ikiwa ni pamoja na kuungana na SBL katika kampeni ya kutoa elimu shuleni kuhusu madhara ya kutumia pombe katika umri mdogo.

Hivi sasa kumeibuka vishawishi vingi kwa vijana vikiwamo vya michezo ya kamari maarufu kama 'betting' na matumizi ya kilevi cha 'Shisha' ambavyo vimesababisha vijana wengi kuingia katika mtego huo.

Sehemu nyingi ambazo Shisha inavutwa ni kwenye baa, hivyo vijana wengi wanaoshiriki wana uwezekano mkubwa wa kushiriki unywaji wa pombe.


Jambo la msingi katika kudhibiti jambo hilo ni kwa viongozi wa serikali, kuanzia ngazi za mitaa, kuanza kupita katika maeneo hayo na pindi wanapobaini kuwapo kwa vijana, wachukue hatua stahiki dhidi yao na wamiliki wa baa.

Kampuni za viywaji zimeweka wazi kuwa watu chini ya miaka 18 hawaruhusiwi kunywa pombe lakini sasa mambo yamebadilika na vijana wa chini ya umri huo, wamekuwa wakitumia vilevi huku hatua zikiwa hazichukuliwi.

Kuna msemo usemao tahadhari kabla ya hatari, hivyo serikali inapaswa kuchukua hadhari kuhusu jambo hili ili kuepusha madhara yanayoweza kujitokeza siku zijazo kutokana na kuwapo kwa vijana wanaotumia pombe katika umri mdogo.

Pia wazazi wanaotumia vilevi, wanatakiwa kuonyesha tabia njema kwa watoto wao kwa kutokunywa pombe hadharani au kuandamana na watoto kwenye maeneo ya starehe hasa ya unywaji wa pombe.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# TANROADS fikeni Mbezi Mwisho mshuhudie namna mnavyohujumiwa

Na Sabato Kasika

**KAWAIDA,** jukumu la kulinda miundombinu mbalimbali inayojengwa na serikali, ikiwamo ya barabara ni la jamii kutokana na ukweli kwamba inachangia ujenzi huo kupitia njia ya kulipa kodi.

Jamii kushiriki katika ulinzi ni la muhimu ni jambo muhimu ambalo linalenga kuifanya miundombinu husika kuwa salama wakati wote bila kuwapo kuhujumiwa.

Ushiriki wa jamii katika ulinzi wa miundombinu ni pale inapoona inahujumiwa na kutoa taarifa kwa mamlaka husika, ili watuhumiwa wachukuliwe hatua za kisheria haraka iwezekanavyo.

Hata hivyo, kumekuwapo na hujuma zinazofanywa na baadhi ya watu, lakini jamii ikiwa kimya, kitendo ambacho kinaonyesha kuna haja ya kuielimisha jamii ili ijue wajibu wa kulinda na kutunza miundombinu.

Moja ya hujuma hizo ni kwenye uzio ulioko pembeni mwa Barabara ya Morogoro eneo la Mbezi Mwisho, Dar es Salaam ambao umeondolewa baadhi ya vyuma ili kuongeza upenyo wa watu kupita.

Kitendo hicho cha kuondoa baadhi ya vyuma ili kupita, kinyume na matarajio ya serikali ya kuweka uzio, waenda kwa miguu wapite juu ya daraja na kujiepusha na ajali za barabarani.

Binafsi ninaamini uzio huo ambao uko pande mbili za barabara hiyo, utakuwa umetumia fedha nyingi za walipa kodi, lakini unahujumiwa huku jamii ikishuhudia lakini ikiwa imekaa kimya.

Hapa ni kama jamii imesahau au haijui kwamba suala la ulinzi na utunzaji wa miundombinu ni la kila mmoja kwa nafasi yake, kwa kutoa taarifa ili hatua za kisheria zichukuliwe pale uharibifu unapofanyika.

Kwa kile kinachoendelea Mbezi Mwisho, ninaomba niwaambie TANROADS kwamba waende eneo hilo washuhudie jinsi kazi waliyoifanya inavyohujumiwa.

Inasikitisha kuona baadhi ya vyuma vimeondolewa kwenye uzio huo, halafu watu wanapenya kana kwamba ni jambo la kawaida au ni haki yao kuhujumu miundombinu hiyo ambayo ni kwa ajili ya usalama wao.

Ikumbukwe kwamba, serikali imekuwa ikiboresha barabara na miundombinu mingine kupitia fedha za nje na hata za ndani ambazo ni kodi za wananchi wenyewe lakini fedha hizo ni kama hazihurumiwi.

Lakini ninadhani ni vyema jamii ikatambua kuwa yenyewe ndio mlinzi wa mali ya umma na umma ndio jamii yenyewe, hivyo haina budi kupambana na hujuma mbalimbali zinazofanywa na baadhi ya watu.

Njia rahisi ni kutoa taarifa pale hujuma zinapofanyika badala ya kukaa, kimya, kwani mtindo wa kukaa kimya unaweza kuwa na mambo mawili, la kwanza likiwa ni kufurahia hujuma au kutoelewa kuwa jamii inahusika kulinda miundombinu hiyo.

Iwapo kuna tatizo la kutolewa umuhimu wa kulinda na kutunza miundombinu, basi ninadhani kuna haja jamii kuelimishwa ili kujua umuhimu huo ili fedha za walipa kodi zisipotee bure.

Jamii pia ingekuwa mstari wa mbele kujivunia miundombinu, kwani ni sehemu ya maendeleo, lakini wanapotokea baadhi ya watu wanahujumu, maana yake ni kwamba hawataki maendeleo.

Hivyo, kwa kuwa sheria zipo, basi hazina budi kuchukua mkondo wake kwa wale ambao wanajihusisha na hujuma huku wakiwa wanajua madhara yake, lakini pia utoaji wa elimu nao ninadhani unahitajika.

Si vibaya TANROADS wakaenda eneo la tukio kurudishia vyuma vilivyoondolewa huku wakitoa elimu kuhusu umuhimu wa kulinda miundombinu ya barabara ambayo imewekwa ili kuepusha ajali.

Ninadhani ushirikishwaji wa wananchi katika kutunza na kulinda hata miradi ya maendeleo ni jambo muhimu, kwani njia hiyo inaweza kusaidia kupunguza hujuma ambazo zimekuwa zikifanywa na baadhi ya watu.

HABARI/SAFU

# TCB yaja na kilimo cha mkataba

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WAKATI Bodi ya Kahawa Tanzania (TCB), ikifikiria kuja na mpango mpya wa uzalishaji wa kahawa kwa njia ya kilimo cha mkataba, bado 'inaumiza kichwa' kutafuta suluhisho la kudumu la vijana wengi kutoingia kwenye mnyororo wa thamani wa zao hilo.

Aidha, TCB imewataka wadau walioko kwenye mnyororo wa thamani wa uzalishaji wa kahawa, kutumia fursa ya pamoja waliyonayo kujadili na kutathimini kwa kina kuhusu changamoto tisa zinazoikabili sekta ya kahawa nchini kwa sasa.

Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Prof. Auleria Kamuzora, amependekeza hatua za msingi zichukuliwe na serikali kupitia Halmashauri za Wilaya zinazolima na kustawisha kahawa kujipanga upya kulifufua zao hilo linalotegemea mauzo yake nje ya nchi kwa asilimia 93.

Prof. Kamuzora alisema hayo jana mjini hapa alipokwenda kuzungumza na wadau mbalimbali na kufungua Tamasha la Kahawa la mwaka 2023.

"Vijana wengi wanaoenda kutafuta kazi ambazo haziwafanyi waende shambani. Mnyororo wa thamani wa kahawa una mambo mengi, wanaweza wakaingia kwenye kuuza, kununua, kukaanga na wanaweza wakawa na coffee shops (maduka ya kahawa) wakafanya kazi.

"Ninaomba tamasha hili liamshe hamasa kwa Wakulima wa Mkoa wa Kilimanjaro kwamba sasa kahawa ni mali. Kahawa inaenda kulimwa kwa kutumia mikataba, inaenda kumuongezea mtu uwezo wa kuzalisha kipato na faida yenye tija kiuchumi," alisema.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TCB, Francis Kajiru, alisema tamasha hilo la siku tatu lililoanza kufanyika Oktoba 27 hadi 29, mwaka huu, ni mahususi kwa wadau wote kusherehekea mafanikio yao, kwa kuwa sekta ya kahawa imeanza kukua na kuonyesha mafanikio tena.

"Tutazitumia changamoto zilizoko kufanya vizuri zaidi, kwa sababu ziko changamoto ambazo bado hazijatatuliwa na kutekelezeka sawa sawa ili kupata suluhisho lake," alisema Kajiru.

Awali, Mwenyekiti wa Jukwaa la Wadau wa Kahawa nchini, Denis Mahulu, akizungumza katika tamasha hilo alisema: "Tuna mpango wa kuongeza unywaji wa kahawa katika eneo la vyuo vikuu na kuanzisha mobile coffee shops (maduka yanayotembea ya kahawa) ambavyo yatawezesha kuongeza unywaji wa kahawa."

Kiwango cha unywaji wa kahawa nchini, kimeongezeka kutoka asilimia tano hado saba huku serikali ikiweka wazi mkakati wake ni kupandisha zaidi kiwango hicho mpaka asilimia 15, ifikapo mwaka 2025/26.

Aidha, wastani wa uzalishaji wa zao hilo la kimkakati nchini, kwa sasa umepanda kutoka tani 50,000 hadi tani 82,000 mwaka huu.

# Mpango akoshwa mipango ya ardhi



**Na Munir Shemweta,** NJOMBE

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, (pichani) juzi alitembelea Banda la Ofisi ya Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Njombe wakati wa hafla ya kufunga Maonyesho ya Nne ya Viwanda Vidogo (SIDO) yanayoadhimishwa kitaifa mkoani hapa.

Akiwa katika banda hilo, Dk. Mpango alielezwa na Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geofrey Pinda, namna wizara inavyotekeleza majukumu katika mkoa wa Njombe ikiwamo umilikishaji ardhi.

"Ofisi yetu ya kamishna hapa Njombe imekuwa ikifanya kazi kubwa ikiwamo kuandaa hati miliki za ardhi na hapa kuna takriban hati 167 ambazo wamiliki wake hawajafika kuzichukua," alisema Pinda.

Akizungumzia ushiriki wa ofisi yake katika maonesho hayo, Kamishna Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Njombe, Fulgence Kanuti, alisema tangu kuanza kwa maonyesho hayo Oktoba 23 , mwaka huu, ofisi yake imeandaa hati milki za papo hapo 18 na wahusika wamezichukua.

Hata hivyo, alisema hati 167 ambazo wamiliki wake hawajazichukua ni za Halmashauri ya Mji wa Njombe na ofisi yake inafanya jitihada mbalimbali kuhakikisha wamiliki hao wanazichukua.

"Mwitikio wa uchukuaji hati milki za ardhi hapa Njombe si mzuri sana kwa sababu naweza kusema watu hapa wako 'busy' ila wanakuja kuchukua pale panapokuwa na uhitaji maalum kama vile mtu akihitaji mkopo benki," alisema Kanuti.

Alisema alisema baadhi ya juhudi zinazofanywa na ofisi yake katika kuhakikisha wananchi wa Njombe wanachukua hati ni kutoa matangazo ikiwemo kutumia redio jamii kuhamasisha.

Kanuti pia alisema ofisi yake inaendelea na kliniki za ardhi katika maeneo mbalimbali na kuweka wazi kuwa mpaka sasa wametembelea baadhi ya mitaa ikiwamo Mgendela, Kihesa, Ramadhani na Kambarage kuwa ni baadhi ya maeneo yaliyotembelewa.

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Siku ya Nyerere itazamwe upya



**Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)**

JULIUS Kambarage Nyerere Burito, ni jina kubwa sana Butiama, Mara, Tanzania, Afrika Mashariki, Kusini mwa Afrika, barani Afrika na duniani kwa ujumla.

Mwalimu Nyerere kama alivyokuja kujulikana baadaye, alizaliwa Aprili 13, 1922 kijijini Butiama wilayani Musoma mkoani Mara na akaja kufariki dunia Oktoba 14, 1999 jijini London, Uingereza.

Baba huyo wa Taifa, amezikwa Mwitongo kijijini Butiama, ambako baadhi ya Watanzania na wasio Watanzania, huenda kuzuru kaburi lake kila wapatapo fursa na kukumbuka mengi aliyowaachia.

Nasi Watanzania wakati anafariki dunia na baada ya kumzika, tuliahidi kumuenzi kwa kutenda na kuendeleza mema aliyotuachia kama jamii, lakini kama wananchi wa nchi aliyoipigania kutoka makucha ya Wakoloni.

Mtanzania yeyote akiulizwa hivi sasa anamuenzi vipi Mwalimu Nyerere, hatakosa la kusema na hasa viongozi ndio kabisa, kwa sababu kuwa karibu tu na Mwalimu hata kinadharia ni karata tosha ya uongozi.

Katikati ya mwezi huu, Watanzania tuliadhimisha miaka 24 ya kumbukizi ya kifo chake, tukiongozwa na Mkuu wa Nchi, Rais Samia Suluhu Hassan kwenye uwanja wa Tanzanite Kwaraa mjini Babati.

Shamrashamra zilikuwa kubwa, kwani zilikwemda sambamba na tukio la kuhitimisha mbio za Mwenge wa Uhuru, lakini pia hitimisho la Wiki ya Vijana. Mbio hizo zilitawaliwa na kaulimbiu ya kuhifadhi mazingira.

Waliohudhuria maadhimisho hayo na hata waliofuatilia kwenye vyombo vya habari, walishuhudia jinsi shughuli za kuzima Mwenge zilivyoshamiri hata kufunika Siku ya Nyerere.

Mapambo yaliyokuwa uwanjani hapo, sare rasmi zilizovaliwa na wahusika wa maadhimisho hayo wakiwamo viongozi wa kitaifa, yalionesha picha za kiongozi mkuu wa nchi, Dk Samia pamoja na Mwenge wenyewe, bila picha ya Nyerere kokote.

Hiyo ni pamoja na mabango yaliyozunguka uwanja huo, ambayo nayo yalikuwa na picha hizo hizo, achilia mbali uwakilishi hafifu wa familia ya Mwalimu, ambao ulifanywa na mwanawe wa kiume, Charles Makongoro.

Mimi binafsi nilitarajia, angalau katika waliopewa fursa ya kuhutubia umati uliofurika uwanjani hapo lakini na Taifa lililokuwa likifuatilia sherehe hizo, basi Makongoro angepewa fursa ya kutoa salamu za familia ya tuliyekuwa tunamkumbuka.

Lakini salamu nyingi ziliegemea kwenye Mwenge na miradi iliyopitiwa nao mikoani katika siku zote ulizozunguka nchini, jambo ambalo ni jema kwa Taifa na ndiyo sababu hata Makamu wa Rais, Dk Philip Mpango akaomba kaulimbiu hiyo iendelee katika mbio za mwakani na unaofuata.

Watoto wa halaiki halikadhalika nao waliegemea zaidi katika kutoa ujumbe wa Mwenge na maendeleo ya mkoa wa Manyara na nchi kwa jumla, bila kujiegemeza kwa Mwalimu na siku yake.

Hivi karibuni, Rais Samia aliunda kamati iliyopitia kujua jinsi Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki inavyojiendesha na kuomba kujua nini kimejiri na hakika alikipata kwenye taarifa.

Mimi nadhani ipo haja kufanya hivyo kwa wizara zingine, lakini hata taasisi za umma, lakini hata hili la Siku ya Nyerere nalo na kupewa uzito ili iwe siku pekee yenye maudhui yanayomhusu Mwalimu kama Mwalimu na si kuchanganywa na mengine na kufunikwa.

Ni kweli, kwamba Siku ya Nyerere ni ya mapumziko, lakini bado hiyo haitoshi kumheshimisha kutokana na uzito na umuhimu wa mchango wake kwa Watanzania, kwani inahitajika siku maalumu, si tu ya kupumzika, bali kukumbuka kwa vitendo aliyofanya.

Tunayakumbukaje? Ndiyo sababu kuna vikundi kama Twende Butiama, kikundi ambacho kwa miaka mitano sasa kimekuwa kikiendesha baiskeli kutoka Dar es Salaam hadi Butiama, humo njiani kikiamshaamsha watu kumkumbuka Mwalimu.

Tuna vikundi vya ngoma, kwaya, bendi za muziki na vingine, vihamasishwe kutunga nyimbo za kukumbuka mema ya Mwalimu na kuimbwa au kupigwa hata kwa wiki kabla ya siku yenyewe, lakini pia kuandaa matamasha, warsha, makongamano, semina na mikutano ya kujadili mema yake.

Lakini kama hayo hayawezekani, tujiulize kwa nini Siku ya Nyerere iwe ya kufariki dunia na si ya kuzaliwa, kama ambavyo watu wengi huadhimisha siku zao za kuzaliwa na si za kufa? Ndiyo sababu hata mataifa husherehekea siku za kupata uhuru au kujikomboa (Taifa kuzaliwa).

Tukiweza hilo, ina maana Siku ya Nyerere itakuwa Aprili 13 ya kila mwaka na hiyo siku ya kifo itaachwa ibaki ya kuzima Mwenge kwa sababu ndiyo siku ambayo na yeye alizima akiwa kitandani katika hospitali ya Mtakatifu Thomas.

Ni ushauri tu ndugu zangu au siyo wajameni!

## UWT yasifu hatua iliyofikiwa makubalino serikali, DP World

**Na Beatrice Shayo**

KATIBU Mkuu wa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Jokate Mwegelo, amesema UWT inaipongeza serikali kwa hatua ya utiaji saini mikataba mitatu ya uwekezaji na uendeshaji Bandari ya Dar es Salaam.

Amesema mikataba hiyo ambayo imeingiwa baina ya serikali na Kampuni ya DP World ni yenye tija na italeta matokeo makubwa kiuchumi.

Jokate aliyasema hayo juzi alipotoa taarifa kuhusu ziara iliyofanywa na Kamati ya Utekelezaji chini ya Mwenyekiti wa UWT, Mary Chatanda, ikilenga kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo nchini.

Alisema mikataba hiyo pia itaifanya nchi kukua kijamii, kibiashara na kuendelea kuimarisha uhusiano kati ya Tanzania na nchi za Falme za Kiarabu.

"Kamati ya utekelezaji UWT imepongeza hatua za serikali kwa kutia saini mikataba ya uendeshaji na uwekezaji wa bandari. Tunaamini ni yenye tija na italeta maendeleo makubwa ya kukua katika sekta ya uchumi," alisema Jokate.

Aliongeza kuwa Novemba 4 mwaka huu, watakuwa na tukio kubwa la kihistoria la kumpongeza Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa kazi kubwa na nzuri ya kuwaleta maendeleo wananchi wake katika kipindi cha miaka mitatu.

Jokate alisema kamati ya utekelezaji imeendelea kuhimiza wanawake na wananchi kwa ujumla walionufaika na mikopo ya asilimia 10 ya fedha zilizotengwa na halmashauri za wilaya, kuirejesha kwa wakati ili kutoa fursa kwa walengwa wengine kunufaika.

Hata hivyo, serikali imesitisha utoaji mikopo hiyo, ikiunda kamati ya kuangalia njia nyingine ya kuitoa baada ya kukumbwa na vikwazo, ikiwamo wakopaji hewa.

"Kamati ya utekelezaji pia inahimiza wazazi kuwajibika katika malezi bora ya watoto ili kukabiliana na mmomonyoko wa maadili hususani suala la ukatili kwa wanawake na watoto ambalo limekuwa changamoto katika jamii zetu," alisema Jokate.

Alisema wanawahamasisha wanachama na wananchi kujiandikisha kwenye daftari la kudumu la mpigakura ili muda utakapofika, wanawake wajitokeze kwa wingi kugombea nafasi mbalimbali za uongozi.

Alisema ziara iliyofanywa imeleta mafanikio makubwa kwa UWT kwa kuongeza wanachama wapya 514,032 na jumla ya mikutano ya hadhara 737 iliyofanyika katika wilaya 62 na miradi 1,284 imekaguliwa katika mikoa 10.

Alisema katika ziara hiyo wamebaini changamoto mbalimbali ikiwamo baadhi ya vijiji kutofikiwa na huduma za umeme, baadhi ya miradi kutokamilika kwa wakati hususani shule na zahanati, upungufu wa watumishi katika baadhi ya sekta kama elimu na afya na uhaba wa maji safi na salama kwa baadhi ya vijiji.

WATOTO NA MITANDAO

# Wataalamu watoa angalizo wazazi, walezi

**Na Vincent Mpepo,** OUT

WATAALAMU wamewataka wazazi na walezi kuwa walinzi wa kwanza wa watoto wao dhidi ya matumizi mabaya ya vifaa vya kimtandao na huduma za mawasilino ili kuwa na jamii inayotambua wajibu na kuthamini maadili.

Ni rai waliyoitoa wakati wa elimu kwa umma kuhusu usalama na matumizi sahihi ya huduma za mawasiliano iliyofanyika hivi karibuni katika Ukumbi wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania na kuhudhuriwa na wafanyakazi wa chuo hicho.

Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA wa Jeshi la Polisi, Kamishna Msaidizi Dk. Dawson Msongaleli, alisema wazazi na walezi wana jukumu la kwanza kuhakikisha aina ya maudhui ambayo watoto wanaangalia, kusoma au kusikiliza, hivyo kujihakikishia udhibiti wa maudhui yasiyofaa.

"Siyo sahihi kumwachia mtoto simu apekue na kuangalia kila aina ya maudhui. Lazima kuwe na udhibiti," alisema Dk. Msongaleli.

Alikosoa jamii kudhani kuwa kwenda na wakati ni kuruhusu watoto kuwa na uhuru uliopitiliza. Ina wajibu kuhakikisha mienendo yao kitabia na kimakuzi inawekewa mipaka ili kuwa na kizazi chenye nidhamu.

Kaimu Mkurugenzi wa Usalama wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Stephen Wangwe alisema elimu inahitajika kwa jamii kutambua namna bora ya matumizi ya huduma za mawasiliano.

Alisema zipo namna za kudhibiti maudhui mtandaoni na kwenye vifaa vya mawasiliano ikiwamo simu janja na kompyuta kwa kuzingatia umri na rika kwa watumiaji, lakini akaweka angalizo kuwa ni wazazi na walezi wachache wana ufahamu na namna hizo za udhibiti.

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Prof. George Oreku aliwashukuru wataalamu hao na kuwaomba kuendelea na elimu hiyo kwa jamii kwa kuwa bado kuna changamoto nyingi za matumizi mabaya ya huduma za mawasiliano.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akisikiliza maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Tanzanite na Sab Gold Ltd, Osman Abdulsattar Tharia (wa tatu kushoto), kuhusu madini yaliyoongezewa thamani alipotembelea banda la kampuni hiyo, katika mkutano wa tano wa madini na uwekezaji Tanzania 2023, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kamati ya Bunge yataka ubunifu vyanzo vipya vya maji Dodoma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Maji na Mazingira imeitaka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) kuendelea kubuni vyanzo vipya vya maji ili kukabiliana na ongezeko la watu jijini.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Jackson Kiswaga alitoa maagizo hayo jana wakati wa ziara ya kamati hiyo ya kukagua mradi wa uchimbaji visima katika eneo la Nzuguni jijini, ambao umefikia asilimia 93. Unaolenga kusaidia kuongeza upatikanaji maji.

Aliipongeza DUWASA kwa utekelezaji wa mradi huo na kutaka iendelee kubuni vyanzo vingine vya maji ili wananchi wapate huduma hiyo kwa urahisi.

Kiswaga aliwahakikishia wananchi waliopisha mradi huo na hawajalipwa fidia kuwa serikali iko hatua za mwisho kukamilisha malipo hayo.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka hiyo, Aron Joseph, alisema utaongeza upatikanaji maji na kunufaisha wakazi zaidi ya 75,000 wanaoishi katika maeneo ya Nzuguni, Ilazo, Kisasa na Jiji la Dodoma.

Alisema kamati imekuwa inafuatilia mradi huo kwa karibu na kuihakikisha kuwa ndani ya mwezi huu wananchi wataanza kupata huduma ya maji wakati wakiendelea kutafuta vyanzo vingine zaidi.

Alifafanua kuwa katika mpango wa muda mfupi, DUWASA inaendelea na utafiti, kuchimba na kuendeleza visima maeneo ya pembezoni mwa mji.


Alisema lengo la mpango huu ni kupunguza adha kwa wakazi katika maeneo hayo na kupunguza utegemezi wa chanzo kikubwa cha Mzakwe.

Aliitaja miradi hiyo ni pamoja na wa uboreshaji huduma za majisafi Nzuguni, miradi wa maji Bihawana, mradi wa maji Zuzu-Nala na uchimbaji visima pembezoni mwa mji ili kupata vyanzo vingine vya maji kwa wakazi wa jiji.

Mwenyekiti wa CCM, Wilaya ya Dodoma Mjini, Charles Mamba, alisema hadi mwakani changamoto ya maji katika jijini humo itakuwa historia.

"Ninaawasihi wanaosimamia mradi wahakikishe thamani ya fedha na matumizi yake inaonekana, ili miradi itekelezeke kwa wakati na wananchi wapate huduma kwa sababu. Dodoma ina watu wengi, hivyo mahitaji ya maji yanazidi kuwa makubwa," alisema.

# MAISHA
OKTOBA 29, 2023
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili


## KATUNIKA

Ukurasa 16


Ukurasa 14



## Maajabu juisi ya ubuyu

## MAISHA NI NYUMBA


Ukurasa 15




# UMEWAHI KUTOKA KIXHOSA AU KIZULU?

Ukurasa 13


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| M | ■ | K | I | U | N | O |
| A | ■ | ■ | ■ | P | ■ | N |
| K | ■ | M | T | U | ■ | D |
| A | G | A | ■ | P | A | O |
| L | ■ | M | B | U | ■ | S |
| I | ■ | B | ■ | ■ | ■ | H |
| O | B | A | M | A | ■ | A |

## FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:


NOA, TIN, DOM, GOA, TANGA, TANDU, AFUTE, NUNDA, SINGIDA, ASIMIKE

## AMSHA AKILI

NI NANI AMEJIFICHA HAPA? TUMIA PENSELI YAKO KUWEKA KIVULI KWA KILA UMBO LILILOWEKWA KIDOA.



## TOA TOFAUTI 5



## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

MTOTO John wakati akiwa njiani kuelekea shuleni, alikutana na kijana mmoja akihangaika kuwasha pikipiki yake kwa kutumia mguu wake wa kulia.

John alimuonea huruma, alikwenda pale alipo kwa ajili ya kumsaidia kusukuma.

John: Habari kaka, nikusaidie kusukuma?

Kijana: Safi tu, hakuna tatizo wewe wahi shule

John: Sawa lakini nakuona uko peke yako

Kijana: Najua mdogo wangu, hiki chombo cha moto huruhusiwi kukichezea

John: Sawa kaka, hata mwalimu alituambia ukali wa moto aujua mpishi

**SWALI**

**Taja sifa ya ndege aina ya popo**

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Kwa nini pombe ni tishio hatima ya vijana wengi?

KARIBU tena msomaji tuangazie unywaji wa pombe. Ni eneo linalotesa sana watu wengi na hasa vijana. Wako waliofikia ulevi wa pombe kupindukia kiasi hata kuwasababishia maruweruwe wakati wote.

Wataalamu wa masuala ya afya wanabainisha kuwa ziko athari za muda mrefu za pombe, wakiainisha faida za kiafya kwa watumiaji wa viwango vya chini vya pombe hadi madhara makubwa katika hali ya matumizi mabaya ya pombe kwa muda mrefu.

Viwango vya juu vya matumizi ya pombe huhusiana na ongezeko la hatari ya ugonjwa wa moyo, kutofyonza vyakula, ugonjwa sugu wa kongosho, ini na kansa.

Uharibifu kwenye mfumo mkuu wa neva na mfumo wa neva za pembeni unaweza kusababishwa na matumizi ya kila mara ya pombe. Matumizi ya pombe kupita kiasi kwa muda mrefu yanaweza kuharibu takribani kila kiungo na mfumo katika mwili. Ubongo unaokua wa kijana aliyebalehe huwa hatarini zaidi kudhurika na sumu ya pombe.

Kihistoria, madaktari wametetea pombe kwa faida zake za kiafya na hivi karibuni kwa ajili ya uwezo wake wa kulinda watumiaji dhidi ya ugonjwa wa moyo. Kuna ushahidi wa faida kwa mishipa ya moyo inayotokana na kutumia kinywaji kimoja hadi viwili kwa siku. Hata hivyo, faida za kiafya kutokana na unywaji pombe kwa wastani ni suala lenye utata.

Baadhi ya wadau wa sekta ya pombe pia wamehusika katika kuongeza chumvi faida za kiafya za pombe. Pombe inapaswa kuonekana kama dawa ya burudani yenye uwezo mkubwa wa kusababisha athari mbaya kwa afya. Haipendekezwi kuwa ulinzi wa moyo badala ya mbinu nyinginezo salama na zilizothibitika za jadi kama vile lishe bora, mazoezi na tiba za dawa.

Baadhi ya wataalamu wanadai kuwa faida za matumizi ya pombe ya wastani zinaweza kupitwa na ongezeko la hatari ikiwa ni pamoja na majeraha, vurugu, uharibifu wa mimba, aina fulani za saratani, ugonjwa wa kongosho na presha.

Kwa vile faida dhahiri za kiafya za matumizi ya pombe ya wastani ni ndogo kwa watu walio katika hatari ndogo ya kupata maradhi ya moyo. Wataalamu wengine wanatahadharisha itumike kwa tahadhari kwa sababu ya uwezekano kwamba, kupendekeza matumizi wastani ya pombe kunaweza kusababisha ongezeko la hatari ya matumizi mabaya ya pombe, hasa miongoni mwa vijana. Manufaa haya ya matumizi wastani ya pombe yanapitwa na hatari za matumizi ya pombe wastani.

Mpenzi msomaji, nimetanguliza hayo ili upate picha ndogo ya kitaalamu kuhusu unywaji wa pombe na athari zake. Yapo maelezo mengi ya kitaalamu kuhusu pombe na madhara au faida katika unywaji wake.

Lakini pia hatuna budi kuzungumzia mifano halisi ya athari za pombe zinazotokana wakati mwingine na tabia inayorithiwa toka vizazi vya nyuma katika baadhi ya familia zenye tatizo hilo.

Hivi majuzi nikiwa ndani ya basi la daladala, niliketi jirani na kaka mmoja. Kidogo akapokea simu akizungumza na jamaa yake. Katika mazungumzo yale, alikuwa akipata taarifa za kijana wao mgonjwa ambaye pombe imemletea madhara makubwa kiafya.

Akawa anamuuliza; amekataa kula. Mbembelezeni tu na hakikisheni geti limefungwa kwa sababu anawazia... Si unajua kila anapokwenda anaacha deni tunafuatwa hapo kulipa?'Msimruhusu atoke, kesho kanisani kwenye maombi".

Mpenzi msomaji, baada ya mazungumzo hayo, ilibidi nimsemeshe jamaa yule. Nikajaribu kumweleza jinsi pepo la pombe lilivyowakamata vijana wengi na jinsi familia zinavyojitahidi kuwanasua lakini wakati mwingine inashindikana.

Kaka huyu akaniambia; "Ni ukweli kabisa, angalia kijana niliyekuwa namzungumzia amemaliza chuo kikuu na alifaulu vizuri lakini kila kazi tunayomtafutia anakubaliwa lakini hadumu kazini. Anaweza kufanya kazi mwezi mmoja lakini baada ya hapo haendi tena kazini, yeye ni kwenye pombe tu.

Amepatiwa kazi sehemu tatu tena zenye mshahara mkubwa lakini kila sehemu akishajionyesha haendi tena. Familia tumekaa tuone namna ya kumsaidia inashindikana. Yawezekana ni ulevi toka vizazi vilivyopita, aidha upande wa mama, baba au bibi na babu zetu", anamaliza kusema ndugu huyu.

Huyo kijana kama siyo pepo la pombe, basi ipo mizimu ya wahenga inayomfuatilia. Fuatilia sehemu ya pili wiki ijayo. ***Je, una kisa cha maisha? Ujumbe mfupi 0715268581.***

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# Ni vyema ukaishi uhalisia wa maisha yako

TOFAUTISHA malengo na vipaumbele vyako. Yaishi mawazo yako maana hakuna aibu wala ushamba, kuyaishi yale uliyoyachagua na kuyapanga kwenye maisha yako.

Kama umeweka malengo ya kufanya vitu fulani mwaka huu, chagua vipaumbele vichache vinavyotekelezeka.

Achana na kurundika vipaumbele sehemu moja, huo ndio ushamba. Malengo yanahamishika kwenda mwaka unaofuata, lakini vipaumbele hubadilika.

Unayumba 'kutoboa' kwenye mipango yako ya maisha, kwa sababu unachanganya mambo.

Sijui unanielewa au niongeze sauti? Anyway, ngoja nianze hivi!. Malengo ni muhimu sana kukuongoza katika safari ya kufikia ndoto uliyo nayo.

Lakini vipaumbele ni kitu ambacho unataka kuanza nacho ili kukupa picha halisi ya kile unachokitekeleza kwa wakati huo.

Ndugu yangu! Hakuna mtu atakayekuja kwenye maisha yako kukutimizia malengo yako, isipokuwa wewe mwenyewe.

Muda unatosha kabisa kutimiza malengo yako, lakini hautoshi kufanya kila kitu kwenye maisha yako.

Kanuni mojawapo ya mafanikio, ambayo unapaswa kuizingatia kama unataka kutoboa katika maisha haya ya sasa, ni kuchukua uamuzi mgumu wa kubadili mwenendo wa maisha yako na malengo yako.

Jizoeze kuwa na vipaumbele vichache kulingana na muda na kipato chako. Si kila ukiamka unakuja na mawazo mapya, mara unataka kununua kiwanja cha ujenzi, wiki ijayo unawaza kununua gari.

Umesahau kuna ada za watoto wako, hukumbuki kuwekeza hata kidogo kidogo, umesahau kabisa familia zetu za kiafrika, nyingi ni tegemezi.

Nikuambie kitu, jikane kwamba sitaki tena kuwatupia lawama watu wengine, ndugu zangu wa karibu, jumuiya nayofanya nayo kazi, ama wana ukoo kuhusu kesi yako ya kushindwa kutimiza malengo yako.

Jiapize kwamba kwangu tabia ya uvivu, visingizo, kughairisha mambo na kuendekeza lawama kwamba wameniotea, wameniloga, wanatembelea nyota yangu, havina nafasi tena kwenye moyo wangu, zaidi ya kuanza kuwajibika kwenye kila hatua ya maisha yangu na malengo yangu.

Rafiki yangu, muda ndio rasilimali pekee ambayo haina mbadala. Ili utimize malengo yako ni lazima uongeze nidhamu ya muda kwenye kupangilia muda wako kuanzia ratiba ya siku, wiki, mwezi na mwaka.

Kingine, marafiki wana mchango mkubwa kwako kufanikisha kutimiza malengo yako au kutotimiza malengo yako.

Kwa hiyo kuwa makini na anza kujihoji, je marafiki zangu ni chachu ya mimi kupambana zaidi kutimiza malengo yangu, au ni chanzo cha mimi kuridhika na kukata tamaa juu ya malengo yangu?

Si mbaya kama ukipambana kuwa na marafiki wenye maono makubwa na wapambanaji, ambao wakati fulani watakuambia ukweli pale unapokosea na kukupa mwanga wa mahali pa kutokea.

Ukichunguza vizuri mwenendo wako, utajikuta ni wewe pekee kwenye kundi la marafiki zako, jumuiya unayofanyia kazi, hau-uishi uhalisia wa maisha yako, unakimbizana na fasheni, kuiga na kufanya mambo nje ya malengo yako.

Hebu amka kwenye huo usingizi mzito wa kufanya mambo kienyeji. Jenga tabia ya kuweka akiba na kufanya uwekezaji hata kama ni mdogo wa ufugaji kuku wa mayai 100 hadi 200 kwa mwaka.

Kufeli jambo fulani katika mwaka fulani, sio hoja ya kushindwa kutimiza malengo yako na kuchagua vipambele vyako vinavyotekelezeka na ukaacha kukata tamaa.

Ndiyo hili ni tatizo kubwa, una pesa kweli lakini kwakuwa huna malengo na unataka kufanikiwa basi unaangalia watu waliofanikiwa na unajaribu kufanya kama wao.

Inakuwaje wewe, kila siku ukiona biashara mpya unafanya, ukiona fulani kanunua gari na wewe unataka.

Ukiona fulani anajenga unaanza kujenga, kanunua kiwanja na wewe unanunua. Yaani hutulii na kufanya kitu kimoja, unafanya biashara tano na zote hazina hata uelekeo.

Hakuna aibu kuuishi uhalisia wa maisha yako. Puuza hisia hasi za kuhofia aibu, jitenge na ulimbukeni wa kupapatikia maisha ya watu wengine.

Ni muhimu zaidi kwenda na muda ulionao kila siku, kwani kumbuka malengo yako ya maisha kiujumla yanategemea zaidi kutimiza kwa malengo yako ya kila siku.Kupanga ni kuchagua!

• **Godfrey Mushi ni Mwandishi Mwandamizi wa Gazeti la Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa barua pepe: ghandsome79@gmail.com Simu ya mkononi: +255 767 535490**

# HARUSI





ILI-KUWA siku ya furaha kwa Lilian baada ya kufanyiwa sherehe ya kicheni pati kwa ajili ya kupewa mafunzo ya kuanza maisha mapya ya ndoa. Sherehe hiyo ilifanyika nyumbani kwao Tuangoma Dar es Salaam wiki iliyopita.



# MITINDO









# UMEWAHI KUTOKA

## Kixhosa au Kizulu?

TOFAUTI za kitamaduni nchini Afrika Kusini zinabainishwa kiufasaha katika aina mbalimbali za mavazi ya kiasili yanayovaliwa na watu wake.

Katika nchi hiyo kuna makabila tisa ambayo ni Wazulu, Waxhosa, Wandebele, Wapedi, Watsonga, Washanga, Wavenda, Watswana, Waswati na Wasotho.

Kila kabila lina vazi lake maalum ambalo hubeba umuhimu wa utamaduni wake.

Wakati dunia inashuhudia mabadiliko ya kijamii, tasnia ya mitindo imeanza kubadilisha mwelekeo wa mavazi hayo ya asili na kuzeweka pamoja na kuwa kivutio.

Kwa mfano mtu anaweza kuchanganya mavazi hayo kwa kutumia kofia ya Kixhosa iliyoundwa maridadi na sketi ndefu ya Imibhaco au Isikhakha isiyo na mpasuko mbele.

Wabunifu pia wameleta mchanganyiko wa kisasa nguo za Kizulu, ikiwamo kofia zenye umbo la duara zinazoitwa izicolo, ambazo huvaliwa na wanawake walioolewa.

Kofia hizi ambazo awali zilitengenezwa kwa nyasi na pamba, sasa zinatumia vitambaa maridadi, ngozi au hariri.

Pia sketi fupi iliyokuwa ikiambatana nayo, mbadala wake yamebuniwa magauni marefu ambayo yamenakshiwa kwa shanga na kuleta mwonekano wa kupendeza.

URЕМBO

Na Mary Geofrey

# NYWELE ZINAZONG'ARA

TUNDA la papai lililoiva ni tiba nzuri ya magonjwa ya nywele na ngozi kama mapunye na mba.

Magonjwa jamii ya mba yanayosababisha ngozi au nywele kukosa mwonekano mzuri na wakati mwingine huleta karaha kwa muathirika kutokana na kuwasha.

Kitaalamu mba ni aina mojawapo ya magonjwa yanayoambukizwa na fangasi ambao husababisha muwasho.

Wanawake wengi wanakumbana na matatizo haya ya mba, kutokana na kupaka vipodozi vinavyowaletea athari katika ngozi zao.

Unapokumbana na tatizo la namna hii ni vizuri kujipaka dawa zinazofaa badala ya kutafuta zile hatarishi.

Mbegu za papai ni tiba nzuri na ya asili ambayo haiwezi kukuletea madhara zaidi.

**Jinsi ya kuondoa mba usoni**

Mbegu za papai ni dawa ya asili inayoweza kutibu ngozi yako na kukuondolea tatizo la kuwashwa au mabaka yanayokukabili.

**Namna ya kutumia**

Unachotakiwa kufanya ni kuzipondaponda na kujipaka kwenye eneo lililoathirika na mba. Hii itasaidia kuondoa ugonjwa huo na kuiacha ngozi yako ikiwa safi na yenye afya nzuri.

Unaweza pia kutumia krimu maalum za kuondoa mba hizo, zinapatikana katika maduka ya dawa, lakini unachopaswa kufanya ni kufuata masharti na kupaka kwa umakini kwenye sehemu iliyoathirika.

Tumia sabuni maalum ya maji, shampoo, poda na hata baadhi ya losheni zinazosafisha ngozi na kuifanya iondokane na muwasho unaokukera.





MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Maajabu juisi ya ubuyu

UNGA wa ubuyu unaelezwa kuwa na vitamini na madini mengi kuliko matunda mengine yoyote unayoyajua.

**Faida zake**

Inaelezwa kuwa unga wa ubuyu una vitamini C nyingi mara sita zaidi ya ile inayopatikana katika machungwa.

Ubuyu una kiwango kingi cha madini ya Kashiamu (Calcium) mara mbili zaidi ya maziwa ya ng'ombe, pia madini mengine yapatikanayo katika ubuyu ni pamoja na madini ya chuma, Magnesiamu na Potasiamu ambayo ni mara sita zaidi ya ile potasiamu ipatikanayo katika ndizi.

Husaidia kujenga neva za fahamu mwilini, ina virutubisho vya kulinda mwili.

Namna ya kuandaa

Chukuwa unga wa ubuyu, weka kwenye kikombe, ongeza maji na ukoroge vizuri chemsha na epua upoe, baada ya hapo ongeza sukari au asali, tikisa na unywe.





MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Haya ndiyo mambo ya kuzingatia utafutapo ardhi kujenga nyumba

KUTAFUTA ardhi ni hatua ya awali ambayo mtu hufanya katika kuelekea kujenga nyumba ya ndoto yake bila kujalisha mahali alipoipata.

Mtaalamu wa ujenzi, Tamiko Hatula, anasema mambo ya msingi unapochagua eneo la kujenga yanayopaswa kuzingatiwa ni pamoja na kufanya uchunguzi wa historia ya eneo husika unalotaka kununua na kuangalia ufikikaji wake.

"Kiwanja chenye barabara pande zote huhusiana na furaha, afya njema na mafanikio, huwa na hewa, mwanga na nafasi ya kutosha. Kwa kiwanja kisichokuwa na barabara pande zote ni muhimu kuwe na barabara upande wa Kaskazini au Mashariki.

"Sababu ya msingi ni kwamba nyumba itakayojengwa itakuwa na mwanga na hewa ya kutosha kuanzia asubuhi," anasema.

Jambo lingine ambalo anashauri kuzingatia wakati wa kutafuta kiwanja kwa ajili ya ujenzi ni pamoja na kuhakikisha eneo unalonunua ni kwa ajili ya makazi au biashara na makazi.

"Hii itakusaidia uepukane na usumbufu wa kubomolewa au kuwa na hofu ya kuhamishwa, hakikisha unafuata taratibu zote za umiliki wa ardhi zilizowekwa," anasema.

Hatula anashauri kuepuka kununua kiwanja kinachouzwa na mtu aliyepatwa na dhiki au kufilisika kwa kuwa baadaye kinachangia kukukosesha furaha na amani.

"Kiwanja cha namna hii ni muhimu kinunuliwe kwa uangalifu mkubwa kwa sababu endapo utanunua kwa lengo la kujinufaisha zaidi, kitakufanya baadaye ukose furaha na amani, manung`uniko yatokanayo na muuzaji au jamii inayokuzunguka yatachangia kukuondolea heshima na utu," anasisitiza.

Anashauri kuepuka kiwanja kilicho jirani au kinachopakana na maeneo ya mikusanyiko mikubwa ya kijamii ikiwamo kumbi za starehe, kanisa, msikiti, kiwanda, chuo, jeshini, shule, soko, sehemu ya stendi za magari.

"Maeneo haya huwa na kelele nyingi na mara nyingi matumizi yake huathiri maeneo yaliyo jirani, ikiwamo kubadilishwa kwa matumizi wakati wowote na pia ni vigumu kulea watoto na kuwakuza kimaadili katika maeneo hayo," anasema.

Mengine anayoshauri kuzingatia ni kuepuka kununua eneo linalomilikiwa au lililomilikiwa na taasisi za kiimani, kuepuka migogoro, lililo jirani na sehemu ya taka, lenye magofu mengi, mapingamizi, chenye nyufa na mipasuko pamoja na chenye udongo wa mfinyanzi.



# Tumia 'nafasi' ya ukuta kunogesha choo chako

**Na Restuta James**

UNADHANI choo chako ni kidogo kiasi kwamba hakipangiliki kabisa? Unahitaji kuboresha mwonekano wake lakini huna namna ya kufanya hivyo? Nifuatilie katika makala haya.

Kama ambavyo dunia inahamia mtandaoni na kampuni nyingi zikipunguza matumizi ya karatasi, basi tasnia ya mapambo imehamia ukutani.

Wataalamu wanaeleza kuwa hakuna sababu yoyote ya nyumba na hususani choo au bafu kutopangiliwa vyema kwa kisingizio cha nafasi ndogo.

Mtaalamu wa mapambo ya ndani Ester Donald, anaeleza kuwa nafasi katika chumba kidogo inaweza kutengenezwa kwa kuongeza ubunifu kidogo.

Akizungumzia bafu na choo, anasema ili kufurahia mandhari ya chumba hiki muhimu, ni vyema kikanakishiwa kwa mapambo asilia kama maua yasiyohitaji mwanga, ambayo yanaweza kutengenezewa nafasi ukutani.


Anasema mbao au chuma inaweza kugongwa ukutani kutengeneza shelf ili kuruhusu uwekaji wa pambo katika chumba hiki.

"Unaweza kuweka maua yasiyokuwa sana na inafaa zaidi yawe yale ya kusafisha hewa, picha nzuri na mdoli. Haipendezi mtu aingie chooni au bafuni akose raha, unaweza kukifanya choo chako kuwa sehemu ya mapumziko," anasema.

Anasema maua na mapambo ya ukutani yanaweza kuwekwa na watu wenye choo au bafu kubwa pamoja na wale wenye vyumba vidogo kama inavyoonekana pichani

Tuwasiliane kupitia restutajames@gmail.com au 0753333330.


# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
MPAKA UNASTAAFU NAFASI YAKO YA UKURUGENZI HUJAWAHI KUWA 'KILAKA' LAKINI HATA KIBANDA HUNA TATIZO NINI?
'VIMINI'
SPOTI
LIVE
KIMATAIFA
ALIYE-TUROGA KAFA!
SISI
MIMI NATANGAZA KIPINDI CHA UMBEA NATAKA UNIPE UBUYU
'WA ZANZIBAR AU WOWOTE?'
MWARABU ANANIJUA MIMI NANI...SASA ZAMU YAKO SIJUI KAMA UTATOBOA!
MIMI SITOBOI BALI NACHANA UPO?
PEKE YANGU NIMETUMBUKIZA KIMYANI BAO TANO!
INGEKUWA PEKE YAKO 'MGANGA' ANGELIPWA?
UNABANA CHIMBO ALAFU DAFTARI LAKO KILA SEHEMU 'VEMA' UNAZITOA WAPI?
MSHUA MBONA USHAJIBU?
AM' SINGO AGEIN!
VITA NI VITA LAKINI SIO VYA KUVISHOBOKEA KAMA NI MKE NTAOA MWINGINE!
*KINYUNYIZO CHA LEO...
NAJUA UNAJUA LAKINI UNAJUA USIOYAJUA...

## HABARI KIMATAIFA

# HAKUNA TENA GAZA

## -Israel yatupa mabomu mazito,
## -Raia wote wapata wasiwasi



Mji wa Gaza ukiwa umetanda miale ya moto na vumbi usiku wa kuamkia jana. **PICHA ZOTE: BBC**

**GAZA,** PALESTINA

NDEGE za kivita za Israel jana zilifanya mashambulizi makali ya mabomu yenye uzito mkubwa kaskazini mwa Ukanda wa Gaza usiku kucha wa juzi na kuibua hofu eneo hilo kufutika kabisa.

Katika taarifa zilizotoka eneo hilo zinaeleza kiwango hicho cha mabomu hakijawahi kushuhudiwa na milipuko yake ilikuwa mikali na yenye sauti ya kutisha.

Mashambulizi hayo yalisababisha eneo hilo kugeuka kuwa vumbi na huku miale ya moto ikitanda eneo zima.

Mwandishi wa BBC, Gaza Rushdi alisema moto ulionekana umetanda angani na kuonyesha Israel ilikuwa imetumia mabomu tofauti.

Madereva wa magari ya wagonjwa walimwambia hawawezi kuwasiliana na mtu yeyote kutokana na hali hiyo, walikuwa wakiendesha gari kuelekea upande wa milipuko kuwanusuru majeruhi.

Alisema kumekuwa na hofu kila mahali, hata mahali alipo Khan Younis, ambako ulipuaji wa bomu ulikuwa mdogo na huku watu wakijaribu kuwafikia jamaa zao katika maeneo mengine kujua kama wako salama, lakini simu zimekatwa.

Taarifa kutoka jeshi la Israel ilisema takriban ndege mia moja za kivita zilitumika katika mashambulizi hayo ya usiku kucha na kuharibu maeneo mengi yanayosadikiwa kuwa ngome za Hamas.

Kulingana na mkuu wa Operesheni ya Jeshi la Anga la Israel Brigedia Jenerali, Gilad Keinan, katika chapisho katika mtandao wa X, vikosi vya Israel vimefanikiwa malengo yake.

"Lengo la jeshi la anga liko wazi kuharibu kila kitu kinachoguswa na mkono wa Hamas," alisema.

Alisema asubuhi ya jana wanajeshi wa Israel wamejikita katika eneo la kaskazini mwa ukanda wa Gaza, katika eneo la Beit Hanoun, na kuelekea upande wa kusini.

Kanda ya video iliyosambazwa jana asubuhi kutoka Gaza inaonyesha jinsi uharibifu ulitokea kutokana na shambulizi kubwa la bomu ambalo halijawahi kushuhudiwa.

Katika hatua nyingine, familia za mateka wanaoshikiliwa ndani ya Gaza zinasema wamekuwa na wasiwasi wakati Israel ikifanya mashambulio makubwa katika eneo hilo.

Katika taarifa iliyotolewa jana asubuhi, familia hizo zinaomba kukutana na Waziri wa Usalama wa Israel na wanachama wa baraza la vita haraka iwezekanavyo.

"Huu ulikuwa usiku mbaya zaidi kuwahi kutokea. Ulikuwa ni usiku mrefu usio na usingizi, kufuatia oparesheni kubwa ya IDF ndani ya Gaza, na tulikuwa na wasiwasi sana kuhusu hali ya mateka wanaoshikiliwa ambao pia ni waathirika wa mashambulizi haya makubwa." Ilisema taarifa hiyo.

Taarifa hiyo ilisema oparesheni ya ardhini inahatarisha usalama wa Walsrael 229 wanaoshikiliwa ndani ya Gaza. "Familia zina wasiwasi kuhusu hatma za ndugu zao na wanasubiri maelezo zaidi. Kila sekunde inavyopita ndivyo wasiwasi unavyozidi kuongezeka. Tunataka Waziri wa Ulinzi, Yoav Gallant na wanachama wa baraza la vita kukutana na sisi asubuhi ya leo(jana)." Ilisisitiza taarifa hiyo

Msemaji wa IDF alisema kuwa kuwarudisha watu waliotekwa ni jitihada muhimu kwa nchi yao na kueleza hatua zote, oparesheni, uchunguzi wa siri, unalenga kutimiza lengo hilo.

Katika taarifa nyingine ya jeshi hilo ilisema limewauwa wapiganaji kadhaa wa Kundi la Hamas katika Ukanda wa Gaza na kuyashambulia kiasi maeneo 150 usiku wa kuamkia jana.

Mkuu wa Kamandi ya Anga ya Jeshi la nchi hiyo Brigedia Jenerali Gilad Keinan alisema ndege zisizopungua 100 zimefanya mashambulizi zikiyalenga mahandaki, vyumba vya chini vya majengo pamoja na miundombinu mingine ya Hamas.

Sehemu ya operesheni hiyo imehusisha pia wanajeshi wa ardhini waliopelekwa kuingia Ukanda wa Gaza siku ya Ijumaa.

Aidha, Jenerali Keinan alisema jeshi linalenga mtandao wa mahandaki ambao kundi hilo limejenga chini ya ardhi.

Alisema ni vigumu kutathmini ukubwa wa mtandao huo wa chini ya ardhi, ambao Israeli inaita "Gaza Metro". Inaaminika mahandaki hayo yalijengwa chini ya eneo la urefu wa kilomita 41 na kilomita 10 kwa upana.

Hata hivyo mashambulizi hayo yamekosolewa kwa matamshi makali na rais Reccip Tayyip Erdogan wa Uturuki, akiitaka Israel ikomeshe kile alichokiita vitendo vya kiwendawazimu.

Kupitia ujumbe kwenye ukurasa wa mtandao wa X, Erdogan alisema mashambulizi ya Israel yameendelea kuwalenga wanawake,watoto na watu wasio na hatia.

Kufuatia mashambulizi hayo, kundi la Hamas limeapa lipo tayari kujibu kwa nguvu isiyo mfano mashambulizi ya Israel.

Kauli hiyo imetolewa wakati jeshi la Israel nalo limetangaza kutangaza kampeni yake ya kijeshi kwenye Ukanda wa Gaza ikijumuisha majeshi ya ardhini.

Kundi hilo la wanamgambo wa Kipalestina linalotawala Ukanda wa Gaza limearifu kwamba wapiganaji wake tayari wanakabiliana na vikosi vya Israel kwenye maeneo ya mpakani.

Wizara ya Afya ya Gaza imetoa orodha ya watu waliouawa tangu kuanza kwa vita hiyo imefikia 7000 kwenye ukanda huo pekee.

**BBC**



Wakazi wa Gaza wakijaribu kujiokoa baada ya jengo lao kulengwa katika mashambulio ya anga.

## MAKALA

# UNAITAZAMAJE NAFASI YAKO YA UONGOZI?



Na Magabilo Masambu

**Mtazamo wa baadhi ya viongozi wetu wa kwamba nafasi zao za uongozi ni za kujipatia fedha au kunyanyasa watu wengine, utawafanya baada ya kifo kukosa majibu mbele ya kiti cha enzi, hivyo mbivu na mbichi zitajulikana huko, tusizitazame nafasi za uongozi kama ajira pekee, bali njia za kuwahudumia watu na hapa ni kila aina ya kiongozi siyo viongozi wa kisiasa tu.**

BAADHI ya viongozi kama si wote hasa katika bara la Afrika, hudhani kuwa nafasi za uongozi ni za kujipatia utajiri na hii ndiyo sababu watu huuana kwa sababu ya madaraka. Madaraka hutafutwa kwa nguvu si kutaka kuwatumikia watu bali ni namna ya kutafuta utajiri binafsi.

Kuna msemo wa Kiingereza unaosema "WHEN YOU ARE LOOKING FOR MONEY, OTHERS ARE LOOKING FOR LEGACY" Maana isiyo rasmi ni kwamba "Wakati wewe unatafuta pesa, wengine hutafuta kukumbukwa na kuenziwa."

Kiongozi mzalendo na wa kweli huwa madhumuni yake si kutafuta pesa, bali hutafuta kukumbukwa ili siku moja atakapoondoka duniani, aache kumbukumbu itakayoishi, maana anatambua hawezi kuishi duniani milele.

Vilevile baada ya kifo chake, huko anakoenda atakuwa na lipi la kumweleza muumba wake juu ya nafasi aliyokuwa nayo duniani kama mtumishi.

Kwa hiyo atakuwa na jukumu la kujitetea kwa nini hakufanya aliyotarajiwa na muumba wake, kuitumia nafasi yake kuwatendea mema watu aliyopewa kuwaongoza.

Mwandishi Mark Cahill anauliza: "When you die, what do you think will be on the other side?" Wakati utakapokufa, unafikiri nini kitakuwa upande wa pili? Ni kweli kwamba hatuwezi kufikiri wakati tumekufa, bali tunatakiwa kufikiri kabla ya kufa kuhusu hatima ya maisha yetu baada ya kifo. Je, kuna maisha baada ya kifo?

Imani zilizo nyingi zinakiri na kuamini kwamba kuna maisha mapya baada ya kifo. Maisha ya kuhesabiwa na kulipwa kadri ulivyoishi duniani kisha kutakuwa na makazi ya kudumu motoni au peponi.

"Msistaajabie maneno hayo kwa maana saa yaja, ambayo watu wote waliomo makaburini wataisikia sauti yake.

Nao watatoka, wale waliyofanya mema kwa ufufuo wa uzima na wale waliyotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu (Yohana 5:28-29). Tiketi ya kwenda peponi au motoni, itategemea maisha uliyoishi duniani. Mwenyezi Mungu alikuumba kwa makusudi ili utimize mapenzi yake.

Mtazamo wa baadhi ya viongozi wetu wa kwamba nafasi zao za uongozi ni za kujipatia fedha au kunyanyasa watu wengine, utawafanya baada ya kifo kukosa majibu mbele ya kiti cha enzi, hivyo mbivu na mbichi zitajulikana huko, tusizitazame nafasi za uongozi kama ajira pekee, bali njia za kuwahudumia watu na hapa ni kila aina ya kiongozi siyo viongozi wa kisiasa tu.

Wanasema uongozi waweza kuwa kipaji wengine wanaita kipawa au karama kutoka kwa Mwenyezi Mungu, hivyo si kila mmoja wetu anaweza kuwa kiongozi, japo wako wengi wasiostahili kuwa viongozi, lakini ni viongozi kutokana na mifumo ya kidunia.

Pepe Minambo aliwahi kusema "You cannot separate leadership from readership" akiwa na maana kwamba huwezi kutenganisha uongozi na usomaji.

Kiongozi mzuri ni yule anayetafuta maarifa. Ukisoma vitabu vingi utapata maarifa na mawazo mengi ya watu mbalimbali, hivyo utaanza kujifunza namna mpya ya kufikiri hatimaye kuwa kiongozi uliyekomaa kifikra na hayo yote yatajulikana katika matamshi na utendaji wako.

Wako baadhi ya viongozi wanaodhani kwamba kuwa na elimu kubwa inatosha kuwa sifa iliyojitosheleza mtu kuwa kiongozi.

Ni kweli kwamba ukiwa umesoma ukawa kiongozi, usomi wako unaweza kukusaidia katika mazingira fulani fulani hasa ya kitaalam lakini si kwamba ni kigezo pekee cha kukufanya uwe kiongozi bora. Ninasema hivyo kwa sababu tumeshuhudia pia baadhi ya wasomi wakubwa kabisa wakifanya mambo ambayo hata ambaye hakusoma anashangaa.

Ni ukweli vilevile kwamba mtu mwenye karama ya uongozi, anaposoma huwa anakuwa kiongozi mzuri zaidi.

Asiyekuwa na karama ya uongozi, hata akisoma bado atafanya mambo ya ovyo katika nafasi yake ya uongozi. Viongozi bora aghalabu huwa ni wale wenye akili na so elimu. Kuna tofauti kati ya akili na elimu, wenye akili ndio walioweka mifumo ya elimu na ndio hufaa kuwa viongozi.

Mara kadhaa nimekuwa nakisikia watu wakisema, fulani amekwenda kusomea uongozi! Uongozi hausomewi, bali watu huenda kujifunza taratibu za kuongoza ndiyo maana kuna wakati kiongozi anapaswa kuweka sheria pembeni na kulijadili jambo kulingana na mazingira na uamuzi wake utokane na mazingira ya jambo hilo.

Niseme tu kwamba mtazamo wa viongozi katika nafasi zenu za madaraka hauna budi ubadilike. Msione kwamba uongozi ni sehemu ya ajira pekee au ya ulaji bali uongozi ni dhamana ya kuwatumikia watu na kwamba unapokuwa kiongozi unakuwa na deni mbele ya muumba wako, maana siku ya mwisho utahitajika kutoa hesabu ya yale yote uliyoyafanya katika nafasi yako ya uongozi na uongozi si uongo.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**Arusha-Tanzania**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Unatembea barabarani kama kichaa, unaumwa na mbu sababu ya mapenzi



Na Adam Fungamwango

**Dk. Remmy Ongalla alishawahi kuimba, mapenzi yana tabaka tatu. Mwanzo wa mapenzi utamu kama chungwa, katikati ya mapenzi uchachu kama limau na mwisho wake ni uchungu kama shubiri.**

MAPENZI ni kama umeme. Ukiwa na umeme ndani ni faraja kubwa kwa sababu utawasha taa, kupikia, kuangalia televisheni, kuchaji simu, utatumia friji kwa ajili ya kuhifadhia chakula na pia vinywaji baridi.

Furaha iliyoje ukiwa na umeme nyumbani mwako. Kama huna utafanya kila njia ili uvute umeme kwa ajili ya matumizi na kukurahisishia maisha.

Lakini umeme huo huo unaweza kuwa ni hatari kwako, familia yao na mali zako. Ikitokea shoti au tatizo lolote linalohusiana na umeme ndipo utakapojua kuwa kwa upande wa pili ni hatari sana.

Unaweza kukuunguzia nyumba, kujeruhi au kuua familia, ikiwemo wewe mwenyewe.

Kwa maana hiyo inabidi uwe mwangalifu mno na umeme kwani licha ya faida zake, lakini kuna hasara pia.

Mapenzi yanafanana na hivyo. Upande wa kwanza ni kitu kinachompa binadamu faraja. Mwanamuziki Maximillian Bushoke, ameshawahi kuimba penzi ni kileo cha fikra. Mtu akipenda au kupendwa huwa anasahau kila kitu kwa muda ule. Anasahau shida zake zote. Anajiona ni mfalme au malkia na watu wote waliobaki wapo chini yake.

Binadamu anatamani kuwa na mbawa aruke juu na kuwatangazia walimwengu jinsi anavyopenda au kupendwa.

Ni wakati ambao mtu haambiwi wala haambiliki. Hakuna anayeona kasoro za mwenzake. Ukimfuata mtu huyo na kumwambia kasoro au tabia mbaya za mwenzake utaonekana mbaya.

Hata ndugu kipindi hicho humuacha ndugu yao baada ya kumweleza ukweli kuhusu mpenzi wake, wanabaki wanamtazama kwa macho na kusubiri nini kitatokea baadaye.

Marijani Rajab naye alishawahi kuimba, penzi linamea popote na mwenye kupenda haoni hatambui, kwenye pengo huona kuna mwanya na kwenye chongo huona kuna kengeza.

Hapo ndipo utakapoambiwa mtu kafa kaoza, kabaki kuzikwa tu.

Hicho ndicho kipindi cha kilele cha juu cha mapenzi ambayo binadamu anapitia.

Lakini binadamu ni binadamu. Wazee wa zamani wana msemo wao kuwa binadamu kilhafu, hakosi uchafu, wakiwa na maana siku zote si malaika, na si mkamilifu kuna siku atakosea tu. Sasa hapo unakuja upande wa pili wa mapenzi. Hapo unaweza kumkuta mtu anatoka nyumbani kwake na ndala, nywele hajachana na kutembea barabarani anaongea mwenyewe.

Kwa sababu yoyote ile, penzi linapogeuka upande wa pili wa shilingi linaumiza na kutesa sana.

Kuna watu wanajuta ni kwa nini walipenda.

Dk. Remmy Ongalla alishawahi kuimba, mapenzi yana tabaka tatu. Mwanzo wa mapenzi utamu kama chungwa, katikati ya mapenzi uchachu kama limau na mwisho wake ni uchungu kama shubiri.

Hayo ndiyo mapenzi ambayo hayajawahi kumuacha mtu salama, uwe tajiri au masikini, msomi na ambaye si msomi, mfanyabiashara na mfanyakazi.

Bendi ya Maquis Original miaka ya 1980 ilirekodi kibao kiitwacho 'Anjelu.' Maudhui ya wimbo huu ni kijana anayemtafuta mpenzi wake bila mafanikio.

Wimbo huu ulitungwa na Kasongo Mpinda 'Clyton' na akashirikiana kuimba na Kikumbi Mwanza Mpango 'King Kiki.' Hebu angalia jinsi jamaa anavyoumia kwa ajili ya mapenzi. Anamsaka mpenzi wake kila kona, lakini haonekani.

"Mapenzi gani yanitembeza barabara yote nakuwa kama kichaa

Kuzunguka vichochoroni kote kumtafuta Anjelu yeye, nachoka nakaa chini nakumbuka siku Alhamisi tulifuatana mimi naye. Usiku wa leo sikulala yoo. Nageukageuka namuwaza yeee. Mbu zinaumiza usisikiee yooo. Mpaka jogoo alfajiri anawika sioni Anjelu yeye.

Jamani sasa Anjelu nasema nataka kukata tamaa, kweli kweli kampatia kisu akate tamaa

Sasa Anjelu nasema nataka kukata tamaa, haki ya Mungu kampatia panga akate tamaa.

Mapenzi gani yanitembeza barabaraka yote nakuwa kama kichaa

Kuzunguka vichochoroni kote kumtafuta Anjelu yeye, nachoka nakaa chini nakumbuka siku Alhamisi tulifuatana mimi naye. Usiku wa leo sikulala yoo. Nageukageuka namuwaza yeee. Mbu zinaumiza usisikiee yoo. Mpaka jogoo alfajiri anawika sioni Anjelu yeye.

Jamani sasa Anjelu nasema nataka kukata tamaa, kweli kweli kampatia kisu akate tamaa

Sasa Anjelu nasema nataka kukata tamaa, haki ya Mungu kampatia panga akate tamaa."

Jamaa anazunguka hadi vichochoroni, haogopi vibaka wala nini, hajali hata mbu zinazomuuma. Anachotaka ni kumuona mpenzi wake tu.

"Ni wangu eee Anjelu ni wangu mama.

Moyo unauma jamani eee, nataka kumuoa Anjelu mpenzi wangu ee

Geuza sura yako nitazame nakosa kiu anjelu mpenzi wangu eee

Mama sogea karibu nichekeshe nipate tuliza moyo wangu eee

Sogea karibu sogea mama. Sogea Anjelu mpenzi wangu.

Mimi naye naye Kasongo naye wangu. Mimi naye naye Kasongo naye wangu.

Anjela eee, Anjela eee, we na Kasongo. Anjela mama ooo, Anjela ya pete na kidole.

Naomba tuoane mtoto wa mama ee.

Ni wangu eee Anjelu ni wangu mama."

Ukiusikiliza wimbo huu utagundua kuwa katika mapenzi bora mpendane wote wawili, au upendwe wewe, lakini ukipenda, tena bahati mbaya pasipopendeka, utatanga na njia.

**Tuma meseji 0716350534**

# HADITHI

CAROLINA, binti mrembo, aliyeumbwa akaumbika, mwenyewe anajiita Carry. Akifahamu fika jinsi alivyo mzuri na kubabaisha kila mwanaume anayekutana naye barabarani, anageuka kuwa mtu mwenye kiburi, jeuri, dharau na majivuno kwa watu. Atamsalimia yule tu aliyempenda kumsalimia. Ataongea na mtu atakayemchagua na si kila mtu. Anaweza kuziba hata pua akipita mtu ambaye yeye anaona si wa hadhi yake. Si mwanaume wala mwanamke. Jirani na anapoishi, kuna kijana mgeni asiyepungua miaka 25 hivi aliyehamia hivi karibu eneo la Kinondoni Moscow. Anaitwa James.

# Kafie kwenu-17

Alikuwa kijana anayeishi maisha ya hali ya chini, akipanga chumba kimoja. Jicho lake naye liliona urembo wa Carry. Akaamua kujaribu. Kilichompata hatosahau maishani mwake. Fuatilia hadithi hii ya kusikitisha, kuhuzunisha, kufurahisha, kuburudisha na kufundisha kwa wakati mmoja.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

FURAHA ya Sauda ilizidi kiasi alipomuona mwenyewe kwa macho yake, mtu ambaye alisikia akisengenywa na kikundi cha wambea wa mtaani kwao akiwemo mama yake kuwa amefungwa jela baada ya kubaka, wengine wakisema aligongwa na bodaboda akafa akazikwa na site, wapo waliosema mji umemshinda ameamua kurudi kwao kijijini.

Zile furaha za watoto zilianza sasa kuwashtua watu wazima, kuanzia kule walikotoka, njiani na hata walipokuwa eneo la tukio.

Walishangaa ni mtu gani anayeshangiliwa na kuwafanya watoto ambao wengi wao ni wanafunzi wa shule za msingi na sekondari kupagawa kwa furaha namna ile?

Mpaka wakati ule hakuna mtu mzima yeyote aliyejua kuwa aliyekuwa anashangiliwa na watoto wa James yule wanayemfahamu.

Baadhi walisikia tu jina la James, lakini hakuna aliyejaribu hata kuhisi kuwa atakuwa ni yule anayefahamika na watu wengi eneo lile ambaye ametoweka pale kwa miaka miwili na nusu.

Baadhi sasa nao walianza kusogea karibu ili kuangalia huyu mtu ni nani?

Kila mmoja alianza kushangaa kivyake walipogundua kuwa aliyekuwa akishangiliwa ni James.


Ndiyo! Yule yule kijana dhalili aliyekuwa akipewa kazi kama kibarua wa mafundi ujenzi, kutumwa mbali kwenda kununua vitu mbalimbali vizito, kutapisha vyoo na makaro machafu, pamoja na kazi zingine ndogo ndogo.

Yule yule, aliyekuwa akikaa kijumba kibovu pake Kinondoni Moscow Bondeni. Kijumba kilichojengwa peke yake kama goli la mpira wa miguu.

Kijumba kilichojengwa kama behewa, kikiwa milango mitatu ya nje, kila chumba kimoja kikiwa na mlango wake.

Kijumba chenye matofali yaliyochoka bila kupigwa lipu, huku juu kukiwa na mabati yaliyobadilika rangi kutoka ya asili na kuwa meusi kwa sababu ya kukaa kwa muda mrefu na kuwa na kutu.

Kijumba ambacho baadhi ya misumari ya mabati yake ilikuwa imeshang'oka na matairi makuukuu yaliyoonekana juu yake haikuwa ni nakshi au urembo bali iliwekwa hapo kwa kazi ya kukandamiza au kuzuia mabati hayo yasing'oke kwa upepo.




**"Jamani amenawiri, amebadilika, kweli dunia hii duara, unayemdharau leo kesho utamheshimu," alisikika mmoja mtu mzima akiongea kwa hisia.**

Kila wakizidi kumuangalia vizuri wanakuta kuwa ni yeye James. Sauti za watoto waliokuwa wakimshangilia na kutaja jina lake zilizidi kuwakumbusha kuwa wanayemuona hapo ni James yule yule wanayemfahamu.

Safari hii alisimama hapo akiwa amenawiri, ngozi yake ikiwa na nuru, wajihi na taswira yake ilionekana hakuwa James yule tena wanayemfahamu.

Ufunguo alioshika mkononi na kusimama kwenye gari alilokuja nalo ilionyesha miaka miwili na nusu ambayo alitoweka pale, alikwenda sehemu ambayo imemtoa sehemu moja kwenda nyingine.

Kutoka ufukara uliotopea hadi kuonekana na gari ilionekana amepiga hatua kubwa ingawa bado wengine wakawa na wasiwasi kama gari ni ya kwake.

Wapo waliokuwa wanamnyanyapaa walioanza kujibaraguza na kumsalimia na kujipendekeza.

Wengi ni wale wale ambao hawakusumbuka kumtafuta wakati alipopotea.

Wakati akiendelea kusalimiana watu wazima, huku wakiwa amezungukwa na watoto rafiki zake, Catty na Carry walikuwa wanarejea kutoka kazini.

James aliposimamisha gari lake ilikuwa karibu kabisa na kina Carry. Wala hakukosea wala kubahatisha. Alisimamisha hapo kimkakati. Alijua pale ndipo kuna watu ambao amewazoea zaidi, nao ni Carry na Catty.

Wakati anashuka chini alipokuwa akiishi alifika kwenye geti, lakini alikuta limefungwa.

Ana uzoefu na hapo, anajua linapokuwa limefungwa kwa komeo na linapokuwa limerudishwa tu.

Walishangaa kuona watu wamejazana karibuni na nyumbani kwao. Walishtuka. Lakini walizidi kusogea karibu.

Katikati ya umati walimwona kijana mmoja mrefu mwembamba. Hata hivyo hawakumtambua.

Hakujua amefanya nini kwani alikuwa amezungukwa na watu wazima na watoto, wengi wao wakionekana na furaha.

Carry ndiye aliyeonekana kuwa na hamu ya kutaja kujua nini kinaendelea kuliko mdogo wake Catty.

"Jamani amenawiri, amebadilika, kweli dunia hii duara, unayemdharau leo kesho utamheshimu," alisikika mmoja mtu mzima akiongea kwa hisia.

Hiyo ilimfanya Carry kuendelea kutaka kujua zaidi. Akazidi kumtazama aliyekuwa anatazamwa na kuzungukwa.

"Kafanya nini kijana wa watu?" Akajiuliza. Lakini kila anavyozidi kumtazama kuna picha ya mtu inamjia.

Ni kama mtu anayemfahamu hivi. "Jamani James," alisikia sauti kutoka kwa mtu mwingine wa karibu yake, ndipo akili yake ikafunguka.

"Ni yeye." Alijiambia mwenyewe baada ya kujidhihirisha. Haraka akahamanika. Akawa kama mtu aliyepandwa na mashetani.

Haraka akaondoka eneo la tukio na kumshtua mdogo wake Catty.

"Dada Vipi Mbona kama umechanganyikiwa, unakimbia nini?"

"Niache, we nenda kamuangalie tu?" Akajibu huku akiwa anazidisha mwendo kuelekea nyumbani. Akafungua mlango na kuingia haraka haraka.

Mdogo wake akaingia na yeye ndani haraka kwenda kumwangalia ndugu yake.

"Una nini wewe?" Akamuuliza tena.

"Nenda kule kamwangalie."

"Nani?"

"We nenda tu."

Carry yeye hakutaka kujihusisha sana kuangalia mkusanyiko wa watu, wala hakuwa na tabia ya kimbea kutaka kujua kila kitu kilicho mbele ya macho yake na asichokiona.

Alipoambiwa tatizo lipo kule, akaamua kurudi kwanza pale kwenye mkusanyiko kuna kitu gani ambacho kimechanganya ndugu yake.

James alikuwa tayari anawaaga majirani zake, akiwaahidi atarejea wiki ijayo. Na alikuwa bado hajawaona rafiki zake, Carry na Catty kwa sababu awali wakati anakwenda kuzulu nyumba yake ya zamani geti lao lilikuwa limefungwa. Ghafla aliona mtu anakuja kwa haraka. Akamtambua kuwa ni Catty. Akatabasamu. Akamuona akiwa anashangaashangaa. James akajiondoa kwenye kundi la watu na kumwita kwa jina, 'Catty!'

Kwa nusu dakika Catty alibaki akimshangaa aliyemwita. Kila akimwangalia anaona sura la James. Lakini si yeye.

"Ni mwenyewe au pacha wake?" Akawa anajiuliza kichwani. Akabaki haelewi nini afanye.

"Catty, ni mimi James, nimerudi!" Akajiweka wazi huku akitanua mikono wake.

Catty akakurupuka na kwenda kumkumbatia. Wote wawili machozi yaliwatoka. Lakini Catty akalia kwa sauti kama ilivyokuwa kwa Salma.

"Ni wewe kweli James. Au macho yangu yananidanganya?"

"Ni mimi. Ndiye James yule yule rafiki yako unayemfahamu. Nimerudi."

**ITAENDELEA JUMAPILI**

# TEMS HANA MPINZANI

MWANAMUZIKI maarufu wa Nigeria, Temilade Openiyi, maarufu kama Tems, amesema hajamuona mtu wa kushindana naye katika muziki.

Amesema kutokana na kukosa mshindani, anachokifanya ni kujishindanisha yeye mwenyewe na anafurahia kuona anapata mafanikio ya kushangaza.

Mwimbaji huyo ambaye ni mshindi wa Grammy na mteule wa tuzo za Oscar amezungumza hayo jana wakati akihojiwa na redio moja nchini Marekani.

"Nina ushindani ndani yangu lakini sishindani na wasanii wengine. Hakuna mtu anayeweza kushindana nami," amesema.

Akasisitiza "Mimi ni asili. Nimekuwa na Watoto, lakini pia, mimi naamini kuwa mwaminifu. Muziki wangu ni wa watu wanaohusiana nao. Kwa hivyo muziki wangu unatoka kwangu. Na muziki wangu ndio chanzo changu.

Ameongeza kwamba alianza kufanya muziki kwa sababu hakuwa na marafiki. Alikuwa na kitu cha kusema lakini hakuwa na mtu wa kumwambia.

"Kwa hivyo, muziki ndio njia yangu. Iwe mtu yeyote ataisikiliza au la, lazima niiachilie. Iwe itafanya au la, sio jambo langu, lakini ninahitaji kuifungua. Na ni kwa ajili ya watu wanaoweza kuungana nao na wanapitia jambo lile lile." amesema.

Tems aliongeza kuwa hajawahi kufikiria kuwa yeye ana sifa zote ambazo amepokea hadi sasa, alisisitiza kwamba alitaka kuimba pekee.



# DJ Gibbz ana ndoto kubwa

MCHEZA muziki anayefanya vizuri kwenye soko la muziki wa Bongo Fleva, DJ Gibbz amesema anatamani kufanya kazi na mastaa wakubwa kwa lengo la kukuza kipaji chake.

Tayari msanii huyo ametambulisha ngoma zake mbili, moja inayoitwa Debbie amefanya na kundi la wasanii kutoka Kenya.

DJ Gibbz amesemna anatamani siku moja kufanya kazi na Diamond Platnumz, Ali Kiba na Marioo kwa njia mbalimbali kama kuwatengezea muziki au kuimba nao.



## ZISIKUPITE

### OSIMHENI KATIKA RADA

LIVERPOOL na Chelsea zipo macho baada ya tetesi kuibuka kuhusu mazungumzo ya mkataba kati ya Napoli na mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Nigeria, Victor Osimhen mwenye umri wa miaka 24, yamekwama. (*Mirror*)

### TAMMY KUONDOKA ROMA

MSHAMBULIAJI wa AS Roma, Tammy Abraham (26), anatarajia kuonyesha nia ya kurejea katika Ligi Kuu England ikiwa Kocha, Jose Mourinho ataondoka katika klabu hiyo ya Italia, huku Chelsea, Aston Villa na Brentford zikiwa tayari zimearifiwa kuhusu msimamo wa mchezaji huyo wa kimataifa wa England. (*Teamtalk*)

### CHIESA ATAJWA SPURS

NEWCASTLE United na Tottenham Hotspur zote zinamfuatilia fowadi wa Italia, Enrico Chiesa na zinaweza kuwashawishi Juventus kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, ambaye mkataba wake unamalizika ifikapo mwaka 2025. (*Calciomercato*)

### CHELSEA YAMTAKA LEABURN

CHELSEA na Brentford zinamfuatilia mshambuliaji wa Charlton, Miles Leaburn mwenye umri wa miaka 19 ambaye ameifungia timu hiyo ya League One mabao sita katika michezo 10 aliyocheza msimu huu. (*Daily Mail*)

### FRED AKARIBIA NEWCASTLE

NEWCASTLE United imemjumuisha kiungo wa zamani wa Manchester United, Mbrazil Fred mwenye umri wa miaka 30, ambaye sasa anachezea Fenerbahce ya Uturuki, katika orodha ya wachezaji wanaotarajiwa kuchukua nafasi ya nyota wa Italia, Sandro Tonali ambaye amefungiwa kwa kipindi cha miezi 10 kwa makosa ya kucheza kamari. (*Fotomac*)

### LOCATELLI ANUKIA EPL

KLABU ya West Ham iko tayari kutoa euro milioni 40 kwa ajili ya kiungo wa Juventus na Timu ya Taifa ya Italia, Manuel Locatelli mwenye umri wa miaka 25. (*Tutto Juve*)

### FENENOORD KUMBANA GIMENEZ

KLABU ya Feyenoord inatarajiwa kudai ada ya takriban euro milioni 100 kwa mshambuliaji wa Mexico, Santiago Gimenez mwemye umri wa miaka 22, ambaye amekuwa akihusishwa na Real Madrid, Tottenham, Arsenal na Chelsea. (*90 Min*)

### KLAPIJA SOKONI ULAYA

ARSENAL imeingia katika kinyang'anyiro cha kumsaka mshambuliaji wa NK Kustosija mwenye umri wa miaka 16, Dino Klapija. Manchester United, Chelsea, RB Leipzig na Borussia Dortmund pia zimeonyesha nia ya kumnunua yosso huyo ambaye amewakilisha Croatia na Marekani katika ngazi ya vijana. (*Daily Mail*)

### LUIZ AWEKWA KIPORO

ARSENAL haina mpango wa kumnunua kiungo wa kati wa Aston Villa, Douglas Luiz ifikapo Januari mwakani, badala yake itasubiri hadi msimu wa joto kuwasilisha dau la kumnunua mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil mwenye umri wa miaka 25. (*Football Insider*)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# ANGE AJIPANGA KUIPA SPURS UBINGWA EPL

**●●●Kocha huyo awaambia mashabiki waendelee na ndoto zao kwa...**

**LONDON,** England

ANGE Postecoglou anawatia moyo Tottenham Hotspur kuota ndoto zao za kutwaa ubingwa baada ya timu yake kupaa kileleni katika msimamo wa Ligi Kuu England kwa pointi tano kufuatia ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Crystal Palace walioupata juzi usiku.

**Bao la kujifunga la Joel Ward na penalti iliyofungwa na Heung-Min Son iliwafanya Spurs kuwa mbele kwa mabao mawili katika kipindi cha pili kabla ya Jordan Ayew goli kufunga la kufutia machozi.**

Postecoglou ambaye ni raia wa Australia alifurahi kusikia mashabiki wao wakiwachangamsha viongozi hao wa ligi.

Aliiambia Sky Sports: "Wacha wawe na ndoto, hiyo ndiyo maana ya kuwa mfuasi wa soka.

"Nina furaha sana leo (juzi). Hapa ni mahali pagumu kufika na tulilazimika kufanya kazi kwa bidii ili kupata ushindi wetu.

Nilidhani tulikuwa na nidhamu ya kweli na umakini kwa hivyo nimefurahishwa na juhudi walizoweka wachezaji wangu. Nilijua ungekuwa mchezo mgumu kwetu."

Palace walitishia muda wote wa mechi na Postecoglou alitoa sifa maalum kwa beki Micky van de Ven, ambaye alikuwa muhimu katika kuwazuia wenyeji.

Mholanzi huyo ameanza vyema Ligi Kuu England na bosi wake alisisitiza yeye ni muhimu kwa mtindo wa uchezaji wa Tottenham.

Alisema: "Jinsi tunavyocheza, tunaihitaji kasi ya Van De Ven.

"Tunacheza kwa ukali sana na safu yetu na kwa kijana mwenye umri wa miaka 22 ametulia.

"Inasaidia kuwa na Romero karibu naye, nadhani anajiamini sana kutokana na hilo. Huo ndio uzuri wake.

"Changamoto kwangu ni hawa jamaa wana mambo mengi zaidi. Ni lazima nihakikishe tunawasukuma na kuwaboresha."

Tottenham watarejea uwanjani baada ya siku 10 watakapomenyana na Chelsea nyumbani.

# JESUS AZIGONGANISHA MADRID NA BARCELONA



**LONDON,** England

KLABU za Hispania, Real Madrid na Barcelona zinadaiwa ziko katika mpango wa kumsajili mshambuliaji wa Arsenal, Gabriel Jesus katika dirisha lijalo la majira ya joto baada ya kuvutiwa na kiwango bora alichokionyesha tangu alipotua kwa Washika Bunduki hao akitokea Manchester City.

Jesus mwenye umri wa miaka 26, msimu huu amefunga mabao manne katika mechi saba za michuano yote, anawindwa na timu hizo mbili kwa sababu umri wake bado unamruhusu na kiwango bora alichonacho licha ya majeraha ya mara kwa mara yanayomwandama.

Timu nyingi zimeonyesha kushawishika na kiwango cha Jesus katika Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa msimu huu ambapo amefunga mabao matatu.

Namna pekee ya Jesus kutua Madrid au Barcelona ni uhitaji wake mwenyewe wa kufanya hivyo, lakinI ikiwa hatoshawishi kuuzwa kuna uwezekano mkubwa Arsenal ikakataa ofa zitakazowasilishwa mezani kwao.

# Mourinho kuondoka Roma

**ROME,** Italia



KOCHA Mkuu wa AS Roma, Jose Mourinho huenda akaondoka katika klabu hiyo mwakani, kwa mujibu wa ripoti kutoka Italia.

Kocha huyo wa zamani wa Chelsea na Manchester United alijiunga na AS Roma mwaka 2021 na kuiongoza kubeba ubingwa wa Europa Conference League katika msimu wake wa kwanza.

Pia aliiongoza kutinga fainali ya Europa msimu uliopita, lakini ameanza vibaya msimu huu na anajiandaa kumenyana na Inter Milan katika mechi ya Serie A itakayochezwa leo.

Mourinho mwenye umri wa miaka 60, bado ana mkataba na AS Roma utakaomalizika mwakani na inasemakana hana mpango wa kubaki baada ya hapo.

Kwa mujibu wa TeamTalk Mourinho yupo mbioni kuondoka baada ya mkataba kumalizika na hiyo inamaanisha AS Roma itaanza maisha mapya bila ya kocha huyo.

Pia imeripotiwa wachezaji kadhaa huenda wataondoka akiwamo staa wa zamani wa Chelsea, Tammy Abraham mwenye umri wa miaka 26.

Mshambuliaji huyo alikuwa usajili wa kwanza wa Mourinho na amefunga mabao 25 katika mechi 75 za Serie A tangu alipotua kikosini akitokea Chelsea alikoonekana kama garasa kwa wababe hao wa Darajani.

Wakati huo huo AS Roma inaamini itamchukua jumla mshambuliaji Romelu Lukaku anayekipiga kwa mkopo kutoka Chelsea wakati wa dirisha la usajili wa majira ya joto mwakani.

# Tonali azivuruga AC Milan, Newcastle

**LONDON,** England

KLABU ya AC Milan huenda ikachukuliwa hatua za kisheria na Newcastle United baada ya kuwauzia, Sandro Tonali ambaye ameathirika na michezo ya kamari kwa mujibu wa ripoti.

Tonali amepatikana na hatia na amefungiwa miezi 10 kujihusisha na masuala ya michezo hivyo Newcastle itapata pigo.

Kiungo huyo wa kati aliyenunuliwa kwa pauni milioni 55 alijumuishwa dhidi ya Borussia Dortmund akitokea benchi Jumatano usiku licha ya kukabiliwa na kesi hiyo na kuambulia kichapo cha bao 1-0 katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Na hiyo ilikuwa mechi yake ya mwisho hadi msimu ujao baada ya kukubali alijihusisha na michezo ya kamari wakati anakipiga AC Milan.

Tonali mwenye umri wa miaka 23 amekubali kufanyiwa matibabu na kuunga mkono kampeni za kupinga kamari hususani kwa wachezaji.

Kwa upande Newcastle United iliapa itafanya uchunguzi kwa kufuata sheria zote kufuatia sakata hilo la nyota huyo wa kimataifa wa Italia na AC Milan.

Na ripoti za Italia zinadai mshahara wa Tonali wa pauni milioni saba unaweza kusikitishwa.

Maswali yamebaki kuulizwa ni kweli Milan ilifahamu Tonali alikuwa anachunguzwa na Mamlaka ya Kuzuia Kamari kwa wachezaji kabla ya kumuuza Newcastle.

Tonali atakosa mechi zilizobaki za kufuzu na michuano ya euro 2024, lakini anatarajiwa kuruhusiwa kufanya mazoezi na Newcastle.



# Azam FC yafunguka ilipoanguka ligi kuu Bara

**Na Saada Akida**

BAADA ya timu yake kupoteza mechi ya pili mfululizo, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Bruno Ferry, amesema wachezaji wake hawakuwa na kiwango bora lakini wataendelea kujifunza kwa sababu bado msimu wa Ligi Kuu Bara unaendelea.

Azam ikiwa nyumbani ilikubali kichapo cha mabao 3-1 kutoka kwa Namungo katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam juzi.

Matokeo hayo yameifanya Azam kuendelea kubakia katika nafasi ya tatu ikiwa na pointi 13 wakati Namungo FC imepanda hadi katika nafasi ya 12 ikiwa na pointi sita kibindoni. Kocha huyo alisema ili kufikia malengo wataendelea kujiimarisha na juzi walikuwa katika wakati mgumu kutokana na kupoteza pia mechi iliyopita.

"Kwanza kabisa napenda kuipongeza Namungo FC, wamecheza vizuri, wameonyesha kiwango bora, walipambana na walikuwa na bahati katika mechi hii, walifanikiwa katika mbinu zao," alisema kocha huyo.

Naye Kaimu Kocha Mkuu wa Namungo, Denis Kitambi alisema siri ya timu yake kupata ushindi ni utulivu waliounyesha wachezaji wake pamoja na kufanya mashambulizi ya kushtukiza.

Kitambi alisema ushindi walioupata utawasaidia sana kupandisha morali na watakaporejea katika uwanja wa mazoezi wataendelea kujiimarisha zaidi.

"Kwa kweli hali yetu ilikuwa, niliwaambia vijana wacheze kwa kutulia, niliwaambia njia ya kutuwezesha kupata matokeo ni kushambulia kwa kushtukiza," alisema Kitambi.

Ligi Kuu Bara inatarajia kuendelea tena kesho kwa JKT Tanzania kuikaribisha Dodoma Jiji FC wakati Prisons itawaalika Geita Gold na Kagera Sugar itawavaa Tabora United.

# NZENGELI : TUNAELEKEZA NGUVU KUIMALIZA SIMBA

**Na Saada Akida**

WAKATI kiungo mshambuliaji wa Yanga kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Maxi Nzengeli akisema anajisikia furaha kuona mabao aliyofunga katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Singida Fountain Gate iliyochezwa juzi yameipatia timu yake pointi tatu muhimu, ameweka wazi nguvu zao sasa zimehamia kujipanga kuifunga Simba.

Nzengeli alifunga magoli mawili katika ushindi wa mabao 2-0 wakati mabingwa hao watetezi walipoikaribisha Singida Fountain Gate katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi.

Ushindi huo uliifanya Yanga ifikishe pointi 18 na kuendelea kukaa kileleni katika msimamo wa ligi hiyo yenye kushirikisha timu 16.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nzengeli alisema alitamani kufunga hat-trick katika mechi hiyo lakini anasikitika hakupata nafasi hiyo.

Nyota huyo alisema anaimani kubwa ya kuendelea kufanya vizuri katika kila mechi na timu yao kufikia malengo wanayotarajia ikiwamo kutetea taji la ubingwa wa Ligi Kuu Bara.

"Tumepata matokeo mazuri, bado tuna michezo mingine mbele yetu, tutahakikisha tunashinda. Ikiwamo mechi ya Simba ambao ni wapinzani wetu katika mbio za ubingwa.

Hizi pointi tatu zimetusaidia na kutuweka katika nafasi nzuri, Singida Fountain Gate wameingia katika mfumo wetu, tunamaliza mechi hii tunaenda kujiandaa na mchezo ujao dhidi ya Simba," alisema Nzengeli.

Aliongeza anaamini wachezaji wote wa Yanga wataendelea kujituma katika kila mechi wanayocheza kwa sababu wanahitaji kumaliza msimu kwa mafanikio makubwa.

"Kikubwa mashabiki wajitokeze kwa wingi kuendelea kusapoti timu yao, tunaimani ya kufanya vizuri kwa sababu tunahitaji kutetea taji la ubingwa, lazima tupambane tushinde mechi yetu ijayo," aliongeza Mkongomani huyo.

Katika mechi hiyo, Nzengeli alifunga bao la kwanza kwa kichwa dakika ya 30 na la pili dakika nane baadaye.

Simba na Yanga zitakutana katika mechi ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu itakayochezwa Novemba 5, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.




Straika wa Azam FC, Iddi Nado (kushoto), akiwania mpira dhidi ya nyota wa Namungo katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam juzi usiku. Azam ilichapwa mabao 3-1. **PICHA: SAADA AKIDA.**

# Uhamiaji, Mlandege hakuna mbabe

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

MAAFANDE wa Uhamiaji wamelazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Mlandege FC katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar iliyochezwa kwenye Uwanja wa Mau A juzi.

Mlandege ndio ilitangulia kupata bao lililofungwa dakika ya 21 kupitia kwa mchezaji wake, Oscar Everest huku Uhamiaji wakisawazisha dakika moja kabla ya kwenda mapumziko kupitia, Yassir Masoud.

Kwa matokeo hayo Uhamiaji imefikisha pointi 11 na kukaa katika nafasi ya nane s a w a na Mlandege FC ambao wanafuatia kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Uhamiaji, Abdul-Saleh Abdallah alisema hayakuwa malengo yake kupata sare katika mchezo huo lakini ugumu wa mchezo ndio umepelekea kugawana pointi.

Abdallah alisema dakika zote tisini zilikuwa ngumu kwa kila upande kwa sababu kila timu ilihitaji alama tatu ili kujiimarisha katika msimamo wa ligi hiyo na kurekebisha makosa ya michezo iliyopita.

"Kipindi cha kwanza hatukucheza vizuri sana, lakini kipindi cha pili kilikuwa chetu, tulikosa magoli mengi ya wazi na kila mchezaji alijitahidi kutumia nafasi yake vyema, tuseme hatukuwa na bahati ya kupachika mabao mengi," alisema Abdallah.

Kocha huyo aliongeza wanaenda kujipanga kwa ajili ya kurejea wakiwa imara katika mechi yao inayofuata dhidi ya Kundemba FC itakayochezwa Novemba 2, mwaka huu.

UK. 22

# Michezo

Jumapili Oktoba 29, 2023

Nipashe



## Jesus azigonganisha Madrid, Barca

# Simba, Yanga zakabana koo

## ●●● Kila moja ina pointi 18, lakini Wekundu wa Msimbazi...

**Na Adam Fungamwango**

JEAN Baleke, straika wa kimataifa kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) na Mzambia Moses Phiri walifunga bao moja kila mmoja na kuipa Simba ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Ihefu SC katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Katika mechi hiyo iliyokuwa na ushindani wakati wote, ilibidi Simba isubiri hadi dakika ya 65 ilipopata bao la pili lililowapa pointi tatu na kufikisha pointi 18 sawa na vinara na mabingwa watetezi wa ligi hiyo, Yanga, lakini timu hizo zikitofautiana mabao.

**Simba jana imefikisha mabao 16 wakati Yanga yenyewe imeshatumbukiza mabao 20 nyavuni.**

Baleke alitupia bao dakika 12 ya mchezo baada ya makosa ya beki wa Ihefu, Vedatus Mwihambi kutaka kumrudishia kipa wake, Fikirini Bakari.

Mkongomani huyo aling'amua mpira unarudishwa nyuma, akapeleka mguu, akaunasa akiwa mita takribani 35 hivi, akaupiga moja kwa moja kwa maarifa hatimaye ukampita Fikirini ambaye alikuwa ametoka na kukwama wavuni.

Straika huyo sasa amefikisha mabao sita, yote akifunga kwa mguu wa kulia, lakini ni bao hilo pekee ndilo alilolifunga nje ya boksi.

Baada ya kuruhusu bao hilo, Ihefu walionekana kubadili mfumo kutokana na kuamua kurudi nyuma ili kupoza mashambulizi ya Simba na kuziba mianya yote.

Hali hiyo iliwafanya wachezaji wa Simba kupiga pasi nyingi ili kutafuta mianya, lakini walinzi wa Ihefu walikaa imara kiasi cha beki wa Msimbazi, Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr' kuamua kupiga shuti kali dakika ya 24 baada ya kuona hakuna nafasi, lakini liliishia kwenye mikono ya Fikirini.

Mfumo huo wa kukaa nyuma na kusubiri mashambulizi ya kushtukiza uliwanufaisha Ihefu sekunde chache tu baada ya Zimbwe Jr kukosa bao, Ihefu ilipata ilifunga goli la kusawazisha kupitia kwa nyota wake, Ismail Mgunda.

Mpira ilianzia kwa Geofrey Manyasi katikati ya uwanja ukapigwa pembeni kushoto kwa Joseph Mahundi ambaye alirudisha ndani kidogo na kumkuta Rajab Athumani akiwa anatazamana na kipa wa Simba, Ally Salim, akaachia shuti kali ambalo lilipanguliwa na kumkuta mfungaji jirani na kuuzamisha.

Kabla ya mabao hayo, Tegere alianza kupiga hodi katika lango la Simba na mapema tu dakika ya nane alipoupata mpira uliopotezwa kizembe akavuta hatua mbili kabla ya kuachia shuti kali lililopanguliwa na Salim na kuwa kona.

Kipindi cha pili kila timu ilifanya mabadiliko kadhaa kwa nyakati tofauti, Simba ikiwatoa, Kibu Denis, Baleke, Clatous Chama na kuwaingiza Luis Miquissone, Phiri, Shaaban Chilunda na baadaye Mzamiru Yassin huku Ihefu iliwaingiza Charles Ilamfya, Nassor Saadun badala ya Mgunda na Tegere.

Phiri aliyeingia kipindi cha pili kuchukua nafasi ya Beleke alipachika baola ushindi ambalo lilionekana kusubiriwa mno na mashabiki wa Simba na kurejesha furaha ya kuondoka na pointi tatu.

Alifunga bao hilo kutokana na kazi kubwa iliyofanywa na Miquissone aliyewalamba chenga mabeki wa Ihefu na kumtangulizia pasi ya upendo mfungaji huyo huku hesabu za Fikirini aliyekuwa ameshatoka kumfuata zikienda kombo.

Linakuwa ni bao la tatu kwa Phiri msimu huu lakini angekuwa makini angeweza kufunga bao lingine dakika ya 80, au kutoa pasi, lakini hakuweza kufanya hivyo na mpira ukatoka nje.



Kiungo wa Simba, Clatous Chama (kulia), akijipanga kumpiga chenga kipa wa Ihefu, Fikirini Bakari katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana. Simba ilishinda mabao 2-1. **PICHA: SIMBA SC**

# Gamondi aelekeza hesabu Msimbazi

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi amesema ushindi wa mabao 2-2 waliopata katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Singida Fountain Gate FC umewaongezea morali wachezaji wake kuelekea mchezo ujao dhidi ya Wekundu wa Msimbazi.

Watani wa jadi, Simba na Yanga wanatarajia kukutana katika mechi ya mzunguko wa kwanza itakayochezwa Novemba 5, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Gamondi aliliambia gazeti hili jana anawapongeza wachezaji wake kwa kupambana na kupata matokeo chanya dhidi ya Singida Fountain Gate na sasa wanatumia mapungufu ya mchezo huo ili kujiimarisha kuelekea mechi ijayo ya dabi.

Kocha huyo alisema ushindi huo ni mwanzo na unawapa nguvu ya kuendelea kujenga kikosi imara kwa ajili ya kusaka matokeo bora dhidi ya Simba.

"Tumefanikiwa kupata alama tatu katika mchezo wa leo (juzi), haukuwa mchezo rahisi, tumecheza vizuri lakini nimeona changamoto na nakwenda kuzifanyia kazi kujiandaa na mchezo ujao.

Mwisho wa mchezo huu ni maandalizi ya mchezo wetu ujao, tunafanya maandalizi kulingana na mpinzani tunayeenda kukutana naye, kwa sasa tunajiandaa kucheza na Simba, ni dabi, tunatakiwa kuwa makini ili kutetea taji hili kwa kufanya vizuri," alisema Gamondi.

Kocha huyo alisema ni mapema kuanza kuzungumzia mchezo watakaocheza lakini sasa mipango yake ni kusahihisha makosa na kujiimarisha ili kutimiza malengo ya kushinda mechi hiyo.

Kocha Mkuu wa Singida Fountain Gate, Ricardo Fereira alisema walihitaji nguvu ya ziada katika mchezo ili wapate ushindi kwa sababu walifanya maandalizi mazuri lakini walishindwa kuondoka na pointi tatu.

Fereira alisema anajua ukubwa wa Yanga, unapocheza na timu kubwa unapofanya kosa unaadhibiwa lakini pia wachezaji wake walikuwa na presha.

"Nimeona baadhi ya maeneo ambayo nitayafanyia maboresho ya kiufundi, dakika ya 20 hadi 25 tulicheza vizuri na kutengeneza nafasi kadhaa, baada ya kufungwa bao akili yetu ikabadilika tukaanza kucheza kwa presha, ingawa tumepoteza lakini nimeridhishwa na kiwango cha wachezaji wangu," alisema kocha huyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >